**MRADI** Bwawa la Nyerere kuibua fursa kiuchumi

UKURASA 2



**MCHECHU** atangaza kiama cha mashirika mzigo kwa serikali

UKURASA 4



Watanzania tunakitesa si kukienzi Kiswahili

Ukurasa 13

DP WORLD NI ZAIDI YA TICTS

Si kuongeza ufanisi ila kufumua uendeshaji 'kienyeji' wa bandari ili kupata tija, maendeleo

Ukurasa 12

BUFE

IJUMAA JULAI 14, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## Umri wa kuishi Mtanzania waongezeka huku idadi ya vijana ikipaa maradufu

Na Sabato Kasika

• Lakini idadi kubwa ni 'jobless'

•UNFPA yataka uwekezaji ajira

MAKADIRIO ya ukomo wa umri wa kuishi kwa Watanzania yameongezeka hadi kufikia miaka 67 na miezi mitatu mwaka jana. Aidha, yanatazamiwa kufikia miaka 74 ifikapo 2035 na hilo litakuwa ni ongezeko la miaka saba na miezi miwili ndani ya miaka 12 ijayo.

Ripoti ya Makadirio ya Taifa ya Idadi ya Watu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaeleza kuwa kati ya mwaka 2013 hadi mwaka 2022, wanaume waliongeza umri wa kuishi kwa miaka minne na miezi sita, wakati wanawake waliongeza miaka mitano na miezi minne, wakiwazidi wanaume kwa miezi minane.

Hata hivyo, asilimia 60 ya Watanzania ni vijana wenye umri wa miaka 24 na idadi ya vijana hao inaendelea kuongezeka.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) zinazotolewa kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Watu Duniani huko Tunguu Zanzibar.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, Bryan Mark Schneiner, anasema zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania wana umri chini ya miaka 24 na kwamba idadi ya vijana inaongezeka, akifafanua kuwa ukuaji huo unamaanisha kuwa uwekezaji wa haraka katika ajira unahitajika.

"Uwekezaji katika ajira kwa vijana, mafunzo ya ufundi stadi, programu za kukuza ujuzi, vitasaidia kuwawezesha kuendesha maisha yao na kuchangia katika malengo ya maendeleo ya taifa," anasema Schneiner.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (wa pili kulia), akiwa na baadhi ya mawaziri wakipata maelezo kutoka kwa Meneja Mawasiliano wa UNFPA, Warren Bright (aliyeshika meza), walipotembelea banda la shirika hilo katika maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani. Kushoto ni Mwakilishi Mkaazi wa UNFPA, Mark Bryan Schreiner. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

Mwakilishi Mkaazi wa UNFPA Tanzania, Mark Bryan Schreiner, akihutubia katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani.

Mwakilishi Mkazi anafafanua kuwa ongezeko la umri linachangiwa na maendeleo katika sekta ya afya ambayo pia yamechochea ongezeko la watu na kwamba kwa mafanikio hayo, kuna haja pia kuwekeza kwenye ajira, ili vijana wawe na kazi.

Ananukuu ripoti ya sensa ya watu na makazi ya 2022 inasema idadi ya watu nchini ni karibu milioni 62, ukuaji wake ni asilimia 3.2 ikimaanisha kuwa katika kila watu 100 wanaongezeka 30 kila mwaka, ambacho ni kiashiria kuwa uwekezaji kwa vijana hauna mbadala.

Anakumbusha kuwa kila Dola moja ya Marekani imewekezwa kwenye uzazi wa mpango, lengo likiwa ni kuboresha afya.

Anasema UNFPA itaendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine kuhamasisha suala la kupata ajira na afya bora hasa kwa wanawake, wasichana na vijana lakini kujua haki zao na kufanya maamuzi yatakayowawezesha kutimiza ndoto zao.

"Tunaipongeza serikali kwa dhamira yake ya kuendeleza rasilimali watu kupitia mikakati mbalimbali na kuwekeza kwenye kusaidia vijana kupata ajira na kuboresha huduma za afya, ukuzaji ujuzi na usawa wa kijinsia na elimu," anasema.

**UKOSEFU WA KAZI**

Ukosefu wa ajira kwa vijana nchini, umeendelea kuwapo, na serikali imechukua hatua mbalimbali zikiwamo kuanzisha programu ya kuwahusisha vijana kwenye kilimo BBT, inayoendelea Bihawana mkoani Dodoma, ikitekelezwa na Wizara ya Kilimo.

BBT inawapa vijana mafunzo, ardhi na mitaji na kuzalisha mazao mbalimbali katika juhudi za kupunguza idadi ya wakosa kazi.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati anasilisha makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/2024 bungeni Dodoma hivi karibuni.

analiambia bunge kuwa viwango vya ukosefu wa ajira kwa vijana bado viko juu na kwamba vinahitaji juhudi zaidi ambazo zitasaidia angalau kuvipunguza.

Waziri Nchemba anakariri utafiti wa nguvukazi wa mwaka 2020/21 kuwa ukosefu wa ajira nchini kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 35 umekuwa ikiongezeka kutoka asilimia 12.1 kwa mwaka 2014 hadi asilimia 12.6 kwa mwaka 2020/2017.

"Tatizo hili la ukosefu wa ajira ni kubwa zaidi hasa kwa vijana wanawake ambao ni asilimia 16.7 ikiwa ni mara mbili ya kiwango kwa vijana wa kiume ambao ni asilimia 8.3," anaeleza Dk. Nchemba.

Anaeleza kuwa kiwango cha ukosefu wa kazi kinaendelea kushughulikiwa na juhudi mbalimbali zinazofanywa ikiwamo uanagenzi ingawa viwango vya ukosefu wa ajira bado ni vya juu na vinahitaji juhudi zaidi kuvipunguza.

Inaendelea Uk 12

# Nipashe

Ijumaa Julai 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581371

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Upigaji mil. 690/- Mahakama Kuu

**WATENDAJI** wadaiwa kuchota fedha za mirathi... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi, akikabidhi tuzo kwa Mwenyekiti wa Maonyesho ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kanali Shija Lupi, baada ya jeshi hilo kuibuka mshindi wa kwanza wa usindikaji wa mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi katika Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. Kulia ni Mke wa Rais, Mama Mariam Mwinyi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 4

## CHANZO CHA WASTAAFU KUFARIKI NDANI YA MUDA MFUPI CHATAJWA

WASTAAFU kuwekeza fedha zao za mafao katika miradi ambayo hawana uzoefu nayo imetajwa kuwa chanzo cha kufariki dunia mapema...

UKURASA WA 4

## SADC YASEMA MSD NI MFANO WA KUIGWA

WAKUU wa Taasisi za Bohari ya Dawa pamoja na viongozi wanaosimamia ununuzi wa bidhaa za afya katika Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), wameeleza kuwa Bohari ya Dawa Tanzania...

## Mwinyi ahimiza uaminifu biashara, uzalishaji kwa tija

UKURASA 3

## Ufaulu Sayansi, Hisabati kidato cha sita waleta matokeo chanya

UKURASA 3

**MICHEZO** CHAMA AITIKISA SIMBA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA



Waziri wa Nishati, January Makamba, aki-waelezea viongozi wa Kanisa la Pentekoste kuhusu mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Upigaji mil. 690/- za mirathi waibuliwa Mahakama Kuu

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara inatuhumiwa kwa ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 695.5 za mirathi katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi 2022. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeithibitishia Nipashe.

Fedha hizo ni zilizowekwa katika akaunti ya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara iliyoko Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa ajili ya kulipwa wategemezi wa mirathi ndani ya mkoa huo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mtwara, Enock Ngailo, alithibitisha jana kuendelea kuchunguza tuhuma hizo. Alisema majalada 55 yaliwasilishwa ofisini kwake. Saba uchunguzi wake umekamilika.

"Majalada saba uchunguzi wake umekamilika na mengine 48 tutakamilisha mwishoni mwa mwezi wa nane (Agosti)...

"Katika kupitia majalada yote haya, tumebaini kiasi cha Sh. 695,574,257.16 (Sh. milioni 695.574) ambazo ziliwekwa katika akaunti ya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara kwa ajili ya kulipwa wategemezi wa mirathi, kimefanyiwa ubadhirifu.

"Ubadhirifu huu umefanyika katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022. Hii mahakama ina akaunti BoT ambayo ni ya kielektroniki. Sasa kwa utaratibu ni kwamba fedha za mirathi zinaingia katika akaunti ya mahakama kutoka benki ambazo marehemu walikuwa wameweka fedha zao. Zinapaswa kulipwa kwa walengwa (wategemezi wa mirathi).

"Sasa, baadhi ya watumishi wa mahakama hasa idara ya uhasibu badala ya kuwalipa yatima na wajane fedha zao, wao walitengeneza wategemezi bandia na kisha kujilipa," alifafanua.

Mkuu wa TAKUKURU huyo alisema kuwa baada ya uchunguzi kukamilika, watapeleka jalada katika mamlaka inayofuata kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria dhidi ya wahusika.

Naibu Msajili wa Mahakama ya Tanzania Kanda ya Mtwara, Fredrick Lukuna, alipotafutwa na mwandishi wa habari hizi, alisema hawezi kulizungumzia suala hilo kwa kuwa hana mamlaka ya kufanya hiyo.

Mtendaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Leornad Magacha, alipotafutwa kwa simu, alimtaka mwindishi kumtumia ujumbe katika simu yake ya mkononi na baada ya kutumiwa ujumbe, alikiri kuwa na dosari hiyo kiutendaji.

Alitaja hatua nne zilizochukuliwa ambazo ni pamoja na kufanya uchunguzi ulioko chini ya TAKUKURU.

"Ndani ya Mahakama, tuna kitengo chetu cha ukaguzi wa ndani, kwa hiyo alipokagua Kanda ya Mtwara ikaonekana kuna mambo ambayo hayaeleweki vizuri ndipo tukashirikisha TAKUKURU wachunguze zaidi. Kwa sasa tusubiri matokeo ya taarifa ya uchunguzi na hatua zao.

"Wananchi (wadaawa) wasiwe na wasiwasi wowote, haki zao za mirathi hazitapotea," alisema mtendaji huyo na kuitaja hatua ya nne - wameongeza umakini katika matumizi ya fedha za umma zikiwamo za mirathi.

**HOJA YA CAG**

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), aligusia fedha hizo.

CAG, Charles Kichere, anasema katika ripoti yake hiyo kuwa alibaini kutokuwapo rejista ya Akaunti ya Mirathi.

Anafafanua kuwa Kanuni ya 131(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 (Toleo la mwaka 2004), inahitaji kiasi kilichopo katika akaunti moja moja za amana mwishoni mwa mwaka wa fedha kuorodheshwa na kufanyiwa usuluhisho na salio lililopo katika akaunti husika za udhibiti.

"Wakati wa ukaguzi wa Mahakama, nilibaini kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, Mahakama kama msimamizi wa mirathi, ilikuwa na jumla wa Sh. 26,656,717,909.04 (Sh. bilioni 26.657) katika akaunti ya mirathi iliyopo Benki Kuu.

"Hata hivyo, hakukua na rejista inayoonesha orodha ya wanufaika wa kiasi hicho; hivyo, usuluhishi wa rejista na akaunti ya benki haukuweza kufanyika kama inavyotakiwa na kanuni za fedha.

"Matokeo yake, ilikuwa vigumu kujua wanufaika wa fedha hizo za mirathi. Kutokana na hilo, ni maoni yangu kwamba menejimenti imekuwa na upungufu katika usimamizi wa fedha za mirathi zilizo chini ya uangalizi wa Mahakama," anabainisha.

CAG Kichere pia anasema aligundua ukosefu wa sheria na kanuni sahihi za usimamizi wa fedha hizo ni sababu ya upungufu huo na kutokana na kukosekana kwa usimamizi sahihi wa fedha hizo za mirathi, kunaziweka fedha hizo katika hatari za kutumiwa vibaya au akaunti hiyo kutumika kufanya miamala isiyoendana na lengo na madhumuni husika.

"Ninashauri Mtendaji Mkuu wa Mahakama kuhakikisha kwamba; kuna sheria na miongozo ya kifedha itakayoelekeza usimamizi wa fedha za mirathi na kuanzisha rejista mtandao ambayo itasajili wanufaika wote wa fedha hizo," CAG anawasilisha hoja yake.

## Mradi wa kufua umeme JNHPP kuinua fursa kiuchumi, uwekezaji

**Na Neema Mbuja,** RUFIJI

VIONGOZI wa Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), wamesema mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), una manufaa zaidi kwa taifa siyo tu kuzalisha nishati hiyo bali utaibua fursa za kiuchumi katika sekta za utalii, kilimo na mifugo.

Mwasisi wa Baraza la Umoja wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania na Mkuu wa huduma ya Wapo Mission International, Askofu Sylvester Gamanywa, alisema hayo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kutembelea mradi huo akiambatana na viongozi wenzake.

Gamanywa aliwahakikishia Watanzania kuwa mradi wa JNHPP ni salama kwa maendeleo ya taifa na kwamba yeye na viongozi wenzake wametembelea maeneo muhimu ya mradi huo na kujionea shughuli zilizokamilika na kuendelea kufanyika.

"Nawahakikishia wananchi kama yalikuwapo majungu kuhusu mradi basi nawaambia CPCT imejiridhisha kuwa mradi ni salama na una faida kubwa kwa Watanzania na uchumi wa taifa. Nichukue fursa hii kuwaambia Watanzania kwamba mradi huu ukikamilika Tanzania itaandika historia nyingine," alisema Gamanywa.

"CPCT tulikuwa tunasikia tu, kuhusu mradi huu, lakini leo tumejionea kazi kubwa imefanyika katika umalizaji wa mradi ulioanzishwa na Serikali ya awamu ya tano," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa CPCT, Askofu Daniel Awet, alishauri serikali kuweka utaratibu wa kufanya ukarabati wa mitambo ya mradi huo, pindi utakapoanza kutoa huduma za uzalishaji wa umeme ili kuwapo na tija zaidi.

Alisema mradi umetumia fedha nyingi, endapo hautakarabatiwa kama ilivyopangwa itakuwa hasara kwa taifa itakayosababisha shughuli kusimama. Pia ameiomba serikali kutumia wataalamu wazawa kuhakikisha wanautunza mradi huo.

Alisisitiza kuwa JNHPP ni mradi mkubwa wa kitaifa wenye manufaa makubwa kwa maendeleo ya taifa, huku akiipongeza serikali kupitia Wizara ya Nishati, kwa usimamizi bora hadi hatua iliyofikiwa ya asilimia takribani 90.

Mchungaji wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, Amon Sikazwe na Askofu Flora Joseph Kaguo kutoka CPCT taifa, walisema wanaishukuru Tanzania kwa maendeleo inayopiga hususani kwenye miradi kama hiyo ambayo utekelezaji wake uko kwenye hatua za kuridhisha sana.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema moja ya faida za mradi huo ni pamoja na ujenzi wa daraja jingine kubwa katika Mto Rufiji ambalo limeshakamilika, akisema kwa siku zijazo wananchi wanaotoka mikoa ya Kusini kwenda Dodoma hawatalazimika kupitia Dar es Salaam badala yake watakatiza katika mradi huo hadi Chalinze.

"Mradi huu una faida katika sekta ya miundombinu ikiwamo ujenzi wa barabara itakayoanzia maeneo Utete mkoani Pwani ili kurahisisha usafiri kwa wananchi wa mikoa ya Kusini na Pwani. Pia mradi wa JNHPP utakuwa na manufaa kwa sekta za maji kwa kuhakikisha huduma hiyo inapatikana kwa urahisi," alisema Waziri Makamba.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
13.07.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumapili tarehe 16-07-2023** kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Arusha** kuelekea **Dar-Es-Salaam Port,** gari hiyo ina namba za usajili: **T 30 EAG / T 232 ABE**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 27.00** |
| **Upana** | - | **mita 3.24** |
| **Kimo** | - | **mita 5.20** |

2. Njia itakayotumika: **Arusha, hadi Dar-Es-Salaam Port kupitia Manyara, Singida, Dodoma, Morogoro hadi Dar-Es-Salaam** Port gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

**HABARI KITAIFA**

## Bil. 731/- kunufaisha wanafunzi 205,000

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, amesema serikali imetenga Sh. bilioni 731 zitazowanufaisha wanafunzi 205,000 katika mwaka wa masomo wa 2023/24.

Kadhalika, amesema serikali imetenga Sh. bilioni 6.7 kwa wanafunzi 1,200 watakaopata ufadhili wa masomo wa Rais Samia Suluhu Hassan (Samia Scholarship).

Kipanga aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua mwongozo wa msimu mpya wa uombaji mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2023/24.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, serikali imeongeza fedha za mikopo ya elimu kutoka Sh. bilioni 570 hadi Sh. bilioni 731 kwa mwaka huu mpya wa masomo utakaonza Oktoba, mwaka huu.

"Idadi ya wanufaika ongezeko hili la fedha limewezesha idadi ya wanufaika wa mikopo kuongezeka kutoka 177,615 mwaka 2021/22 hadi 205,000 wanaotarajiwa kupata mikopo ya elimu ya juu mwaka huu mpya wa 2023/24.

Aidha, alisema Samia Scholarship ilianza kwa mara ya kwanza katika mwaka wa masomo uliopita kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu zaidi katika masomo ya sayansi katika mitihani ya kidato cha sita ambao wanaendelea kusoma shahada za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati au afya.

Kipanga alisema katika mwaka uliopita, wanafunzi 593 walipata ufadhili huo wenye thamani ya Sh bilioni 2.75 ambazo zinagharimia masomo yao kwa asilimia 100. Alisema kwa mwaka huu mpya wa masomo serikali imetenga Sh. bilioni 6.7 kwa ajili ya wanafunzi 1,200 watakaopata ufadhili huo.

Pia alisema katika kipindi cha miaka mitatu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeboresha mifumo yake na kuiunganisha na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili kurahisisha huduma za uombaji mkopo.

Kipanga alifafanua kuwa dhamira ya serikali kuwawezesha vijana wa kitanzania kupata elimu ya juu inaonekana kwa vitendo.

"Kwa hiyo, tukisema Mheshimiwa Rais anaupiga mwingi, mnatuelewa kazi inaendelea," alisema.

Kapinga alisema uombaji mkopo kwa mwaka huu una maelezo ya kina kuhusu sifa, utaratibu wa kuwasilisha maombi ya mkopo kwa usahihi na namna ya kufuatilia ombi lako kwa njia ya mtandao kupitia Student's Individual Permanent Account (SIPA).

## Ufaulu Sayansi, Hisabati kidato cha sita waleta matokeo chanya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la Mitihani Tanzania (NECTA), limetangaza matokeo ya kidato cha sita huku ufaulu wa masomo ya Sayansi ukiwa ni asilimia 44.95 na wa jumla ni 99.23.

Akitangaza matokeo hayo kwa mwaka huu visiwani Zanzibar, Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Ali Muhamed, alisema watahiniwa waliofanya mitihani yao walikuwa 106,883 na waliofaulu ni 104,549 sawa na asilimia 99.23.

Alisema kwa mwaka 2022 watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa 93,136 sawa na asilimia 98.97 na kwamba ufaulu wa jumla umeongezeka kwa asilimia 0.26 ikilinganishwa na mwaka 2022.

Katibu huyo alisema kati ya watahiniwa waliofaulu, wavulana wanaongoza wakiwa ni 57,842 sawa na asilimia 99.00, ikilinganishwa na wasichana ambao walikuwa 46,707 sawa na asilimia 99.51.

"Watahiniwa wa shule waliofaulu ni 96.010 sawa na asilimia 99.90 ya watahiniwa wenye matokeo, mwaka 2022 walikuwa 84,404 sawa na asilimia 99.87 hivyo ufaulu wa watahiniwa wa shule umeongezeka kwa asilimia 0.03 ikilinganishwa na mwaka 2022," alisema Katibu huyo.

Upande wa watahiniwa wa kujitegemea waliofaulu mtihani huo ni 8,539 sawa na asilimia 92.30 na mwaka 2022 walikuwa 8,732 sawa na asilimia 91.11 na kwamba kwa mwaka huu kiwango kimeongezeka kwa asilimia 1.19.

Aidha, alisema ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata watahiniwa wa shule unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa 95,442 sawa na asilimia 99.30 wamepata ufaulu mzuri wa daraja la kwanza hadi la tatu na watahiniwa wengi wamepata daraja la kwanza na la pili ambao ni 36,527 sawa na asilimia 38.01.

Hata hivyo, alisema ubora huo wa ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu ni mzuri zaidi kwa wanafunzi wavulana, ikilinganishwa na wasichana na kwamba wavulana ni 52,463 sawa na asilimia 99.36 na wasichana ni 42,979 sawa na asilimia 99.24. Dk. Said alisema ubora wa ufaulu wa daraja la kwanza kwa wavulana ni mzuri zaidi kuliko wasichana na wavulana waliopata daraja hilo ni asilimia 40.57 na wavulana ni 34.88.

Alisema wanafunzi 11 wamefutiwa matokeo yao ya mitihani kwa sababu ya udanganyifu na walioshindwa kufanya mitihani yao kwa sababu mbalimbali ikiwamo za kiafya ni 169.

Aidha, Baraza hilo limeendelea na utaratibu wake mpya wa kutotangaza shule, wanafunzi bora na walioshika nafasi ya mwisho.

## Mwinyi ahimiza uaminifu biashara, uzalishaji kwa tija

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi ametoa wito kwa wazalishaji wa ndani na wafanyabiashara kufanyabiashara zenye tija na kuhudumia mahitaji ya oda wanazopatiwa kwa uaminifu na kuzalisha bidhaa zenye viwango na ubora unaohitajika.

Akizungumza jana wakati wa kufunga Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa mkoani Dar es Salaam jana, alisema wote wanafahamu jinsi masoko ya biashara yalivyokuwa na ushindani baada ya kuingia katika eneo la soko huru la Afrika.

Alisema hivi sasa wigo wa biashara umepanuka huku akiwasihi Watanzania kutumia fursa hizo kupata masoko ya bidhaa zao katika maeneo ambayo wananufaika nayo yakiwamo ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Nawasihi Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) ihakikishe inaendelea kufanya utafiti wa uhakika wa masoko mapya ya bidhaa zetu na kuutoa kwa wafanyabiashara wetu," alisema na kuongeza;

"Pia natoa rai kwa wadau wote kuongeza uzalishaji wa bidhaa ambazo zinahitajika katika masoko ya ndani na nje ya nchi kama sukari, mafuta ya kula, unga wa ngano na bidhaa za ujenzi ikiwamo saruji ili kujitosheleza kwa matumizi ya ndani na ziada tuuze nje," alibainisha Rais Mwinyi.

Pia, alizitaka taasisi zinazosimamia biashara kuondoa urasimu na kuwezesha za ndani zaidi, huku akiwahakikishia kuwa serikali zitaendelea kushirikiana kuhamasisha ukuaji wa biashara na uwekezaji kwa kufanyia kazi maoni ya wafanyabiashara.

Kwa mujibu wa Rais Mwinyi, serikali zote zina dhamana ya dhati kuboresha zaidi mazingira ya biashara nchini kwa kuwezesha taasisi za serikali kuwa na mifumo inayosomana inayoweza kupunguza gharama za biashara zisizo za lazima na kuondoa utitiri wa tozo.

Mkurugenzi wa TanTrade, Latifa Khamis, alisema idadi ya washiriki katika maonyesho hayo imeongezeka hadi 3,500 mwaka huu kutoka 3,200 ya mwaka 2022, na kwamba kati ya hao wa ndani ni 3,240 na wakigeni ni 260.

"Hadi kufikia jana watembeleaji zaidi ya milioni tatu walifika katika maonyesho haya, makubaliano tisa yaliingiwa ya ushirikiano wa kibiashara ikiwamo ununuzi wa pamba ya Tanzania tani 30,000 kwa mwaka baina ya Bodi ya Pamba na kampuni kutoka Algeria," alisema na kuongeza;

"Pia washiriki wa maonesho haya waliuza bidhaa zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 3.8 ukilinganisha na bilioni 3.6 za mwaka 2022, TanTrade itaendelea kusimamia na kuratibu shughuli mbalimbali za kibishara na kuhakikisha sekta hii inaendelea kukua, kuimarika na kutoka mchango wa ajira na kuongeza pato la taifa," alisema Latifa.


**COMMUNITY DEVELOPMENT TRUST FUND**

**TAARIFA KWA UMMA**



***Hubert Henry Sangu***

Bwana **Hubert Henry Sangu** mwenye picha hapo juu anatafutwa na polisi RB Na. **CDS/RB/2619/2023** kwa tuhuma za kumuibia mwajiri wake **CDTF Tanzania.** Yeyote atakayemuona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taasisi haitahusika na makubaliano yeyote atakayoyafanya kuanzia tarehe ya Tangazo hili.

**Community Development Trust Fund**
**P.O.Box 9421**
**Dar es salaam**

21749602

# Mchechu atangazia kiama mashirika mzigo

**Na Romana Mallya**

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu, amesema mpango wa kuboresha mashirika ya umma 298 unatarajiwa kuanza mwaka huu.

Katika maboresho hayo, mpango huo pia utabainisha mashirika yatakayofutwa, yatakayounganishwa na mengine kuwekwa kwenye angalizo maalum.

Hatua hiyo inatokana na agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alilotaka kufanyika tathmini ya utendaji wa mashirika yote ya umma na yale ambayo serikali ina hisa kubwa, kuyabaini yasiyo na faida ambayo yameshindwa kujiendesha na yanaitia hasara serikali hasara.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika mkutano uliohusisha ofisi yake, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na wahariri, Mchechu alisema yako mashirika ambayo mabadiliko yake yataonekana ndani ya mwaka mmoja au miwili na mengine kwa kipindi cha miaka mitano.

Akizungumzia agizo la Rais, alisema kwa sasa wako kwenye hatua za mwisho kwa sababu walitakiwa kuboresha kidogo kilichofanyika awali.

"Kinachofanyika ni kwamba kuna taasisi ambazo majukumu yake yanaingiliana au yanajirudia.

Hizi tutaziunganisha ili tuwe na ufanisi mzuri. Ziko taasisi ambazo ni muhimu lakini zimekuwa zikifanya vibaya, hizi tunaziweka kwenye angalizo maalum kwa kuzipa jicho la karibu kuhakikisha zinabadilika.

"Kuna taasisi ambazo hazifanyi vizuri na pia zimepitwa na wakati. Hizi tunakwenda kuzifuta. Zile ambazo unaziona zinayumba lakini bado zina mahitaji tutaziboresha kuwasaidia mameneja walipo wasiposaidika tutatafuta wengine.

"Haya maboresho tunakwenda kuyafanya, yataanza mwaka huu na yatatuchukua miaka miwili kuonekana ya umuhimu wake. Kuna taasisi ndani ya mwaka mmoja au miwili matokeo yake yataonekana na zingine zitahitaji kujengwa mpaka miaka mitano," alisema.

Mchechu alisema kati ya taasisi ambazo ofisi yake inazisimamia, 248 zinamilikiwa na serikali kwa asilimia 100 na zingine inazimiliki kwa ubia.

"Taasisi zote 298 zina mtaji wa zaidi ya Sh. trilioni 70 na ni taasisi muhimu kwa sababu zinagusa huduma muhimu za maisha ya Watanzania," alisema huku akibainisha kwamba Rais Samia alizungumza kwenye hadhara akitaka wafanye mabadiliko ya utendaji wa taasisi za umma.

"Tunatamani hizi taasisi za umma zifanye kazi kama zile za sekta binafsi. Hakuna sababu Mchechu afanye vizuri sekta binafsi halafu kwenye taasisi ya umma unashindwa.

"Au leo tukawachukua kina Ruth (Zaipuna) wa NMB (Ofisa Mtendaji Mkuu) na Abdulmajid (Nsekela) wa CRDB (Mkurugenzi Mtendaji) halafu tukasema wanashindwa. Watashindwa kwa sababu ama hatujawatengenezea mazingira mazuri, hatujawawezesha au hakuna utamaduni wa kupimana," alisema.

Mchechu alisema katika mabadiliko wanayokwenda kuyafanya ni pamoja na kupeana malengo na kupimana na kuhakikisha kuna kuwa na watu sahihi wanaokwenda kuziongoza kwa kuwapa uhuru wenye uwajibikaji na kuwezeshwa rasilimali.

Alisema lengo ni kuongeza mchango wa taasisi katika pato la taifa ndani ya miaka mitano ufikie asilimia 10 ya bajeti ya nchi kutoka asilimia tatu na baadaye wafikia asilimia 20.



Wakazi wa Kitongoji cha Bwiti, Kijiji cha Kimbo, Kata ya Potwe, wilayani Muheza mkoani Tanga, wakiwa wamepanga foleni kwa ajili ya kupiga kura za kumchagua diwani wa kata hiyo, kwenye uchaguzi mdogo jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Chanzo cha wastaafu kufariki ndani ya muda mfupi chatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WASTAAFU kuwekeza fedha zao za mafao katika miradi ambayo hawana uzoefu nayo imetajwa kuwa chanzo cha kufariki dunia mapema.

Kwa kufanya hivyo husababisha kupata matatizo ya kiafya yakiwamo shinikizo la damu kutokana na uwekezaji wao kushindwa na kusababisha wengi wao kufilisika.

Mstaafu wa mahakama mkoani hapa na mmiliki wa mgahawa wa Chapati Chapati jijini hapa, Sharif Kasmili, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika hafla ya uzinduzi wa mgahawa huo.

Alisema kutokana na wastaafu wengi nchini kuwekeza fedha zao kwenye miradi ambayo hawana uzoefu nayo baada ya kustaafu kimekuwa chanzo kikubwa cha vifo vyao.

"Wastaafu wengi miradi ambayo wanawekeza fedha zao za mafao ni ile ambayo hawana uelewa nayo ndiyo maana unakuta wengi wanakufa kutokana na presha kutokana na miradi hiyo kufa na wao kufilisika," alisema.

Alisema ili kuondokana na tatizo hilo, watumishi wa umma wanapaswa kuanzisha miradi yao kabla ya kustaafu, ili wawe na uzoefu nayo na kujenga maisha yao ya baadaye.

"Lazima watumishi wa umma kuwa na miradi ambayo itakusaidia baada ya kustaafu ambayo tayari unaifahamu na kuiendesha badala ya kusubiri hadi ustaafu unaweza kufa kwa presha kwani itakufa na kiasi chote cha fedha za mafao kitakwenda na maji," alisema.

Mstaafu huyo aliwataka Watanzania kuchangamkia fursa zilizoko hivi sasa mkoani Dodoma ikiwamo uwepo wa Ikulu ya Chamwino, Bunge pamoja na mji wa serikali.

"Watu hatupaswi kuendelea kulalamika kuwa hali ni ngumu bali tutumie fursa ya uwepo wa ongezeko la watu mkoani hapa kufungua miradi kama hii ya migahawa na mingineyo ili kutoa huduma itakayokidhi mahitaji ya ongezeko hilo la watu mkoani hapa," alisema.

Pia aliishauri serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wazawa ikiwamo kuwapunguzi riba kwenye mikopo, ili wapate mitaji watakayoitumia kufanya uwekezaji mkubwa.

Aliipongeza serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa ubunifu wa mradi wa jenga kesho iliyo bora (BBT) ambao utasaidia vijana kupatiwa mashamba, mbegu, mafunzo na nyenzo muhimu ambazo watazitumia ili kujikwamua kiuchumi.

# SADC yasema MSD ni mfano wa kuigwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKUU wa Taasisi za Bohari ya Dawa pamoja na viongozi wanaosimamia ununuzi wa bidhaa za afya katika Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), wameeleza kuwa Bohari ya Dawa Tanzania (MSD) ni mfano wa kuigwa katika nchi hizo.

Aidha, wamesema MSD itakuwa chachu ya kuunganisha maendeleo na kukuza uchumi wa Afrika kutokana na ufanisi wake katika upatikanaji wa uhakika wa dawa na bidhaa za afya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya kufanyika kwa mkutano wa siku mbili wa viongozi hao, uliofanyika nchini, Mwenyekiti wa wakuu hao, Richard Biayi, alisema wameona shughuli zinazofanywa na MSD na wameridhishwa nayo na wanaamini siku chache zijazo Afrika itashikamana hasa katika eneo la uagizaji bidhaa za afya.

Pia, wakati wakiwa MSD wametembelea ghala la kuhifadhi dawa na bidhaa za afya na kushuhudia uzalishaji wa barakoa kwenye kiwanda cha MSD kilichopo kwenye bohari hiyo na walichojifunza Tanzania imepiga hatua kwenye eneo hilo.

Viongozi hao wapo nchini tangu Julai 10 kwa ajili ya kikao cha kujadili na kuboresha namna ya kununua dawa kinachotarajiwa kumalizika leo.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, alisema kuwa uwapo wa viongozi hao kutoka SADC imelenga kukutana na kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu maboresho ya kimfumo katika uendeshaji Bohari ya Dawa.

"Ni kama tunabadilishana uzoefu na kila mmoja anajifunza, mfano wenzetu Zambia ni wazuri sana kwenye nishati mbadala kwa hiyo ni vyema kujifunza ili nasi siku zijazo tupunguze gharama," alisema.

Aliongeza kuwa mkutano wao wa mkakati wa ununuzi dhidi ya viongozi hao wa SADC ulihudhuriwa na nchi zote za jumuiya hiyo na ambao hawakuwapo walishiriki kwa njia ya mtandao na wametoka na mapendekezo kadhaa.

"MSD na Sekretarieti ya SADC tumejadili namna ya kuboresha ununuzi na tumetoa mapendekezo ya muda mfupi, wa kati na mrefu," alisema.

Vile vile, alisema wamependekeza namna ya kuboresha mfumo wa ununuzi na kuboresha bidhaa za afya, usimamizi, rasilimali watu na fedha, malipo na mawasiliano.

"Mfano, mfumo unatakiwa wa kidijitali maana tuko nchi mbalimbali hatuwezi kuwasiliana kwenye makaratasi... mapendekezo yakikubaliwa, vipaumbele vitawekwa na tutakwenda kwenye utekelezaji," alisema Tukai.

TANGAZO

# UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

CARING FOR FAMILY ECONOMY

## DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014
## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES ( GHARAMA ZA HUDUMA ZETU KUFIKIA TAREHE 30.06.2023)

| REVIEWED CHARGES | | |
|---|---|---|
| **DEPOSIT RATES** | | **RATES** |
| Savings Account **(p.a)** | | 1% |
| Mavuno Account - Special Deposit Account (p.a) | | 9% |
| **Fixed Deposit** | | |
| 3 Months | | 4% |
| 6months | | 5% |
| 12Months | | 6% |
| Negotiable rates for Amount Exceeding 50Mil | | 6% to 7% |
| Negotiable rates for Amount Exceeding 100Mil | | 8% to 9% |
| Negotiable rates for Amount Exceeding 500Mil | | 10% |
| **CHARGES AND FEES** | | |
| **ITEM/TRANSACTION** | | **CHARGE/FEE** |
| **Current Accounts** | **USD** | |
| Minimum Opening balance - Company and individual | 50.00 | 100,000.00 |
| Monthly Statement enquiry | 2.00 | TZS 1,500 per month and TZS 700 for extra page |
| Monthly Ledger fee | 10.00 | 15,000.00 |
| Account closing charges | 10.00 | 20,000.00 |
| Sale of bankers cheque | | 30,000.00 |
| Cancelation of bankers cheque | | 30,000.00 |
| Cheque book per leaf | 0.18 | 400.00 |
| Stop payment order | 10.00 | 30,000 reported lost/stolen cheque book/leaf (per notice) |
| Standing order within the bank per entry | 2.00 | 1,000.00 |
| Standing order to other banks per entry | 20.00 | 15,000.00 |
| Confirmation of Balance and Audit statement | 25.00 | 50,000.00 |
| Salary processing fee per entry | N/A | 2,000.00 |
| Upaid cheque (RD) | 40.00 | 40,000.00 |
| Montly fees - Parishes Account | N/A | 5,000.00 |
| - Other Current Account | N/A | 15,000.00 |
| Quartely fees - Other Current account | | 2,000.00 |
| Deposit fee | N/A | free |
| Withdrawal on current account using cheque | | Up to TZS 400,000 TZS 1,500, 400,000.001 to 5,000,000 TZS 2,000 from 5,000,000.001 above 0.05% max 150,000 |
| **Savings Accounts** | | |
| Minimum Operating Balance | Mavuno Saving Account | 5,000.00 |
| | Uchumi Account | 10,000.00 |
| | Personal Saving | 20,000.00 |
| Account closure | | 20,000.00 |
| Dormant account reactivation | | free |
| Withdrawal fee over the counter | 1% of the amount | Up to TZS 400,000 TZS 1,500, from 400,000.001 to 5,000,000, from 5,000,000.001 to 10,000,000 TZS 2,000 from 10,000,000.001 to 50,000,000 TZS 10,000,000 from 50,000,000 TZS 0.05% max TZS 150,000 |
| Account maintenance fee - Monthly | | 1,500.00 |
| - Quartely | | 1,600.00 |
| Bulk Cash deposit | | free |
| New ATM card issuance | N/A | 10,000.00 |
| ATM card renewal or replacement | N/A | 15,000.00 |
| ATM withdrawal fee | | 1,300.00 |
| PIN Reset ATM | | 5,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | **Electronic Banking** | | |
| | SWIFT/TISS transfer | | 11,800.00 |
| | Mobile banking balance enquiry | | 200.00 |
| | Transfer from bank account to mobile | | |
| | Mobile - PIN reset | | 2,000.00 |
| | **Other Charges** | | |
| | Cheque clearing fee (Outward Cheques) | | 1,000.00 |
| | EFT | | 2,000.00 |
| | Search fees (including vouchers) | | one month free, 2 to 6 months 20,000, above 6months 50,000. CCTV footage 30,000 max 6months |
| | Uncollected cheque book (after notification) | | TZS 2,000 per month |
| | Coins deposit | | 3% of the deposited amount (non parish) |
| | Brela Search Fees | Company Limited | TZS 25,000 |
| | | Trade name | TZS 7,000 |
| 4 | **Internet Banking** | | |
| | 24/7 Transfer UCB to UCB | | Free |
| | 24/7 Transfer (Other Banks) | | 11,800.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 1,000 -100,000 | 2,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 101,000-200,000 | 3,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 201,000-500,000 | 5,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 500,1000-1,000,000 | 6,000.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) | Tzsh 1,001,000-2,000,000 | 8,500.00 |
| | 24/7 Airtime processing | Payment | free |
| | 24/7 Government payment | | free |
| | 24/7 Other payments (utility) | DSTV, Star Times, AZAM, Water Bills etc. | 1,500.00 |
| | Balance inquiry | | Free |
| | Monthly fee per retail user | | 1,500.00 |
| | Monthly fee for corporate user | | 2,500.00 |
| | Retail & Corporate subsricption | | Free |
| | Bank statement self download | | 500.00 |
| | Cheque book request 100 leaves | | 47,200.00 |
| | Cheque book request 50 leaves | | 23,600.00 |
| | PIN Regeneration | | Free |
| | Salary processing | | 1,800.00 |
| | Standing Order Instructions | | 2,000.00 |

Prepared : (Supervisor) .........................

Checked : (Manager) .........................

Approved by: (GM) .........................

217495502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe kudhibiti matukio watu kuuana, kujiua

**MATUKIO** ya watu kujiua kwa sababu mbalimbali yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara nchini kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu hizo ni madai ya kuwapo kwa hali ngumu ya maisha, wivu wa kimapenzi, migogoro ya mali katika ndoa na mzigo wa madeni.

Hivi karibuni, kwa mfano, jijini Zanzibar, mwanamke mmoja ameripotiwa kujiua kwa madai ya kuzidiwa na mzigo wa madeni kutokana na kukopa fedha nyingi kutoka vikundi vya kuweka akiba na kukopa, maarufu kama VICOBA. Kabla ya kuchukua uamuzi huo, mwanamama huyo alishaaeleza ndugu zake kuwa atafanya hivyo kutokana na kuzidiwa na mzigo wa madeni lakini wakadhani anafanya mzaha.

Licha ya tukio hilo za Zanzibar, kuna matukio mbalimbali yaliyoripotiwa kuhusu watu kujiua kwa sababu ya madeni wanayodaiwa na VICOBA. Miongoni mwa matikio hayo yaliripotiwa kutokea katika mikoa ya Arusha, Iringa, Tanga, Lindi na Mtwara.

Mbali na matukio hayo ya kujiua kutokana na madeni yanayotokana na mikopo kutoka benki au vikundi vya VIBOBA, wako watu pia waliokatisha uhai kwa sababu zingine kama vile kukosekana kwa uaminifu na uwazi katika matumizi ya fedha.

Mfano mmojawapo ni mwanamume mmoja mwaka jana aliyejiua baada ya mke wake kutumia fedha walizokuwa wameziweka kwa ajili ya kununulia runinga. Lakini jambo la kusikitisha ni lile lililotokea nchini Kenya la mwanamume kujiua kisa mke wake alikataa kumpikia kuku! Wivu wa kimapenzi umechukua nafasi kubwa ya watu kuuana na kujiua katika maeneo malimbali nchini. Miongoni nmwa matukio hayo yamechangiwa na baadhi ya wanaume kuwatuhumu wenza wao kuwa wana uhusiano na wanaume wengine, hivyo kuwasaliti katika ndoa au mapenzi. Hatua hiyo imesababisha maafa makubwa ndani ya baadhi ya familia kwa baadhi ya wanaume kuwaua wake zao na watoto kisha na wao kukatisha uhai wao.

Tatizo hili pia limekithiri katika baadhi ya taasisi za elimu ya juu kwa kuwa huripotiwa mara kwa mara kuwa baadhi ya wanafunzi wa kike wamekuwa wakichukua uamuzi wa kujiua baada ya kukataliwa na marafiki zao wa kike. Hata wanafunzi wa kiume pia wamekumbwa na madhila kama hayo kutokana na kukataliwa.

Mfano mmojawapo ni tukio lililotokea Januari, mwaka huu kwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) kujinyonga kwa madai ya kukataliwa na mpenzi wake. Kijana huyo, ilidaiwa awali alimlipia kodi mpenzi wake huyo na kumnunulia simu janja lakini baada ya siku chache alikataliwa kwa kile kilichoelezwa kuwa msichana huyo alimwambia amempata mwanamume mwingine.

Hayo ni matukio machache kati ya mengi ambayo yamekuwa yakitikisa hata kupewa nafasi za juu katika vyombo vya habari. Kukithiri kwa matukio hayo, kunadhihirisha kwamba tatizo ni kubwa, hivyo hatua madhubuti zinapaswa kuchukuliwa.


Ni wakati mwafaka sasa kwa wadau mbalimbali wanaohusika na masuala ya saikolojia, maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na viongozi wa serikali, kimila na dini kuingilia kati kabla ya tatizo kuota mizizi. Kikubwa ni kuwapo kwa elimu na unasihi kuhusu kudhibiti msongo wa mawazo, kuyapokea mambo yanapofika na kuomba ushauri pale inapotokea hivyo.

Katika vyuo kwa mfano, ni wakati mwafaka wa kuwapo na makundi mbalimbali ya waelimisha rika na ushauri kwa vijana wanapoingia katika uhusiano wa kimapenzi na kupewa tahadhari kuhusu hatari zinazoweka kutokea pindi uhusiano unapovunjika.

Viongozi wa dini pia wanapaswa kutenga muda wa kuzungumza na makundi maalumu kama vile vijana wa marika mbalimbali, wanandoa na watu wazima wakiwamo wastaafu kuhusu namna ya kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza kwenye muktadha mzima wa uhusiano na msongo wa mawazo. Ni dhahiri kwamba iwapo kila mmoja katika nafasi yake na zamu yake atachukua hatua, suala la mauaji katika familia na watu kujiua kutokana na sababu mbalimbali linaweza kupungua kwa kiasi kikubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Utaratibu mpya mikopo uwadhibiti wafujaji

**HISTORIA** inaonyesha kuwa utaratibu wa utoaji mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ulianza rasmi mwaka 1993 baada ya serikali kutafakari na kuona umuhimu wa kuwezesha makundi hayo muhimu ndani ya jamii ambayo hata hivyo ni maskini kupindukia.

Katika kufanikisha utaratibu huo, serikali ilianzisha Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana, ili kuwapa mikopo wanufaika hao na kuwawezesha kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara, na uzalishaji wa bidhaa.

Hata hivyo, ndani ya safari hiyo, imekutana na vikwazo mbalimbali vikiwamo vya walengwa kukosa mikopo na pia kuwapo kwa utafutanaji wa fedha za walipokodi unaodaiwa kufanywa na baadhi ya watumishi.

Kutokana na mazingira hayo, ndipo serikali ikaamua kusitisha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 iliyokuwa ikitolewa na halmashauri, baada ya kubaini kuwapo kwa madudu, hadi hapo utaratibu mwingine utakapoelekezwa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ndiye aliyetangaza kusitisha mikopo hiyo Aprili 13 mwaka huu, akihitimisha hoja yake ya makadirio ya bajeti kwa mwaka 2023/24 bungeni jijini Dodoma.

Hakuweka wazi zuio hilo linakwenda hadi lini, lakini ninaamini hatua iliyochukuliwa na serikali, inalenga kuwasaidia walengwa ili waondokane na adha waliokuwa wakiipata, aidha, kuwadhibiti watumishi wa halmashauri waliokuwa wakijinufaisha kwa fedha hizo.

Wakati huu ambao serikali inajipanga ili kuja na utaratibu mpya, ingependeza kwa kuwa utakuwa ni mwiba kwa 'mchwa' ambao umekuwa ukitafuna fedha za halmashauri ambazo ni kodi ya wananchi.

Si siri kwamba kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wakopaji na hata wabunge kuhusu jinsi ya ukopeshaji huo, huku ikidaiwa kuwa baadhi ya walengwa hukosa mikopo hiyo.

Wakati wakopaji wanalalamikia ukopeshaji uliojaa milolongo, urasimu, kukwamishwa hata Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imewahi kusema fedha hizo zinaliwa na wajanja na kusababisha kukosa mwendelezo wake.

Waziri Mkuu ameshafafanua kuwa kuanzia fedha ambazo zimerejeshwa Aprili mwaka huu hazitakopeshwa tena, zikitakiwa kusubiri utaratibu mwingine kwa kadri itakavyoelekezwa.

Binafsi ninaunga mkono hatua zilizochukuliwa na serikali, ili kuokoa kodi za Watanzania ambazo zimekuwa zikiishia mikononi mwa watu wachache na kusababisha walengwa kuendelea kuumia kwa kutafuta mikopo mingine yenye masharti magumu.

Kwa mfano, huko mitaani kuna mikopo imepewa majina yakiwamo ya 'roho mkononi' kwa sababu ya masharti ya urejeshwaji wake, hivyo wanalazimika kwenda kukopa huko mitaani, ili waendeshe biashara zao kutokana na ugumu wanaokutana nao kwenye halmashauri.

Uamuzi wa serikali wa kusitisha mikopo ya halmashauri, ni kwamba inataka kuandaa utaratibu mzuri wa ukopeshaji wa fedha hizo kupitia benki, ili kuwasaidia zaidi wahitaji.

Ninadhani ingekuwa ni vyema kama utaratibu unaoandaliwa na serikali utaharakishwa, ili wanawake, vijana na watu wenye ulemavu waondokane na adha ya 'mikopo umiza au roho mkononi'.

Kilichokuwa kikifanyika ni kama wananchi walikuwa wamezingirwa na maumivu, kwani kupata mikopo kwenye halmashauri ni shinda, wakienda kukopa mitaani nako shida zaidi.

Sasa wamebaki wakisburi utaratibu mzuri wa ukopeshaji wa fedha hizo kupitia benki, ambao ulitangazwa na serikali, hivyo kama inawezakana, basi utaratibu huo ungeharakishwa.

Kwa ujumla benki ndizo zinazotarajiwa kufanyakazi kwa ubora na ufanisi zaidi hasa kwa kudhibiti ukopaji wa kibabaishi.

Kuna madai kuwa wapo wanaokopa na kuazimia kuwa hawatalipa kwa sababu fedha imetolewa na kiongozi wao wa kisiasa aweza kuwa diwani, mbunge au mwenyekiti wa chama.

# HABARI KITAIFA

## Mradi wa majisafi wanufaisha vijiji vinne

**Na Faustine Feliciane, aliyekuwa**
TARIME

KAMPUNI ya uchimbaji dhahabu ya Barrick umetumia zaidi ya Sh. milioni 900 kufanikisha mradi mkubwa wa majisafi na salama unaonufaisha vijiji vinne katika Wilaya ya Tarime.

Pia imefanikisha uzalishaji wa maji safi na salama na ujenzi wa tangi kubwa la kuhifadhi maji lenye uwezo wa kubeba maji lita 300,000.

Katika ziara ya kuangalia mradi huo wilayani Tarime hivi karibuni, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumiaji Maji Wilaya ya Tarime, Dotto Lino, alisema mradi huo uliowezeshwa na Barrick, kwa sasa unanufaisha vijiji vinne vya Mwatongo, Nyangoto, Nyabuhire na Mjini Kati.

"Mradi huu umeshakamilika na kaya zaidi ya 3,700 zenye watu zaidi ya 34,000 zinanufaika na mradi huu wa maji ambao umesaidia sana wananchi wa vijiji hivi hususani kinamama ambao walikuwa wanatembea umbali mrefu kufuata maji," alisema Lino. Alisema mpaka sasa kuna vituo 21 katika vijiji vyote kwa ajili ya mabomba ya kuchotea maji kutoka kwenye tangi hilo kubwa lilojengwa Matongo.

"Kukamilika kwa mradi huu kumesaidia kupunguza bei ya maji kwa ndoo. Hapo awali maji tulikuwa tunanunua mpaka Sh. 500 kwa ndoo, lakini kupitia mradi huu wananchi wananunua maji kwa Sh. 40 tu kwa ndoo," alisema Lino.

Pia alisema wameanza kuwaunganishia maji wananchi majumbani mwao kwa gharama nafuu na kuwawezesha kupata huduma hiyo katika maeneo yao.

"Kuna maombi 300 ya wananchi wanaotaka kuunganishiwa maji na mpaka sasa kuanzia Mei mwaka huu tumeshawaunganishia maji watu au kaya 65. Kaya hizi, zinachangia huduma kwa Sh. 2,000 tu kwa uniti moja ambayo ni sawa na ndoo 1,000," alisema Lino.

Meneja Msaidizi wa Idara ya Uhusiano wa Kampuni ya Barrick, Hermrnce Christopher, alisema baada ya kukamilisha ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji, mradi huo wameukabidhi kwa serikali ya wilaya kwa ili uendelezwe.

Alisema serikali ya wilaya ndiyo itapanga taratibu za namna bora ya matumizi ya mradi huo mkubwa wa maji.

"Kwa sasa, baada ya kuukamilisha kwa asilimia 98 mradi huu, tunaanza mchakato wa kusambaza maji haya kwa vijiji vingine saba vilivyopo hapa Tarime Vijijini. Kwa sasa ni vijiji vinne tu vilivyounganishwa na mradi huu," alisema Christopher. Aliongeza kuwa maji hayo yanatokana na shughuli za uchimbaji mgodini. Maji mengi yanazalishwa na mgodi. Wameamua kuyakusanya maji hayo na kuyatibu na kuyatumia katika matumizi ya kawaida ya binadamu.

"Kwenye shughuli zetu za uchimbaji chini ya ardhi tutazalisha maji, sasa mgodi umejenga mitambo ya kusafisha maji hayo na kuyarejesha kwenye matumizi ya kawaida. Maji haya ndiyo tunayoyatumia wafanyakazi wa mgodini," alisema Christopher.

Alisema kuwa kabla ya mradi huo wa kusambaza maji kwa wanakijiji kupitia mabomba, kampuni hiyo ilikuwa inasambaza maji kwa kutumia magari yake kwa wanavijiji wa karibu na mgodi huo.



Mkurugenzi Mtendaji wa SGA, CPA Eric Sambu (wa pili kushoto), Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, ACP Mtatiro Kitinkwi (katikati) na Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya SGA, Oscar Mgaya (wa pili kulia), wakionyesha cheti cha ubora chenye nambari ISO 18788 ambacho SGA imekuwa ikitunukiwa kwa miaka mitatu sasa ikiwamo mwaka huu, katika hafla ya kuwaaga wastaafu wa kampuni hiyo na kuwaenzi waanzilishi, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tanzania ina uhaba wa nyumba milioni 3.8

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuangalia namna bora ya kutumia teknolojia ya kisasa katika ujenzi wa nyumba ili kujenga nyumba nyingi na kwa muda mfupi.

Vilevile, waziri huyo amebainisha kuwa nchi ina uhaba wa nyumba milioni 3.8, hivyo kunahitajika kujengwa walau nyumba 500,000 kila mwaka ili kukabiliana na uhaba huo.

Dk. Mabula aliagiza hayo juzi alipokagua ujenzi wa mradi wa nyumba uliopewa jina la Samia Housing Scheme, unaotekelezwa na shirika hilo huko Kawe mkoani Dar es Salaam.

"Tunahitaji kujenga nyumba siyo tu kwa kutumia matofali tuliyonayo bali kuwa na teknolojia nyingine itakayotuwezesha ujenzi wa nyumba nyingi na kwa muda mfupi, lakini nyumba imara," alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Waziri Mabula, nchi zilizoendelea ziko katika hatua nzuri kwa kuwa ndani ya mwezi mmoja zinaweza kujenga nyumba 20 na NHC inatakiwa kupiga hatua kwa kuangalia mabadiliko hayo.

Dk. Mabula alisema kuwa mwaka ujao (2024), Tanzania itakuwa mwenyeji wa maonesho ya kimataifa ya tekonolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na itajifunza kwa wengine.

Pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na serikali kuliwezesha shirika hilo kukopa fedha za kuendelea na miradi iliyosimama kwa muda mrefu.

Serikali iliipa rukhsa NHC kukopa Sh. bilioni 173.9. Hadi sasa shirika hilo limekopa Sh. bilioni 44.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Akielezea zaidi kuhusu uhitaji wa nyumba nchini, Dk. Mabula alisema katika sensa iliyopita, takwimu zinaonesha kuna uhitaji wa zaidi ya nyumba milioni 3.8 na kama ujenzi utafanyika kwa kasi, zitahitajika kujengwa nyumba 500,000 kila mwaka.

"Bado kuna uhitaji mkubwa wa nyumba na sehemu kubwa ya nyumba zinazojengwa na shirika letu la NHC watu wameonesha nia ya kuzichukua na kwa mujibu wa sensa iliyopita, upo uhitaji mkubwa wa nyumba katika Jiji la Dare es Salaam," alisema Dk. Mabula.

Alikumbusha kuwa kupitia bajeti ya mwaka huu wa fedha (2023/24), wananchi sasa watanunua nyumba za gharama nafuu kwa kuwa wameondolewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa nyumba yenye thamani isiyozidi Sh. milioni 50.

Kwa kutambua hilo, Dk. Mabula alisema serikali sasa inahakikisha nyumba zinajengwa kwa wingi ili Watanzania wazinunue.

Alitoa rai kwa watu wenye fursa ya kuendeleza ujenzi, kufanya hivyo kwa kuwa uhitaji wa nyumba ni mkubwa nchini.

NHC ilibuni mradi wa nyumba 5,000 za gharama nafuu wa Samia Housing Scheme zitakazojengwa kwa awamu katika mikoa mbalimbali nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 466. Kwa kuanzia, shirika lilianzisha ujenzi wa nyumba 560 Kawe mkoani Dar es Salaam.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**






Ofisa Mauzo wa Kampuni ya GF, Juma Lukolo (wa pili kushoto mbele), akitoa maelezo kuhusu ubora wa magari aina ya Honh Yang yanayotengenezwa na kiwanda cha kuunganisha magari cha GFA Kibaha mkoani Pwani, kwa wafanyakazi wa kampuni hiyo waliotembelea maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waajiri waona tija michango yao WCF

**Na Halfan Chusi**

WAAJIRI wamesema fedha wanazochangia katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) hazipotei kwa kuwa kuna maslahi ya pande tatu - mwajiri, mfanyakazi na serikali.

Kwa nyakati tofauti katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, maarufu Sabasaba yaliyofikia kilele jana, waajiri hao walipongeza serikali kwa kuanzisha mfuko huo kwa kuwa unatoa hakikisho la usalama kwa mfanyakazi.

"Tayari tumeanza kuchangia, tuchukue nafasi ya kuelimishana ndani kwamba iko fursa ndani ya WCF kutoa hudumia kwa wafanyakazi pindi wanapokumbwa na madhila kazini," alisema Akbarali - mwajiri kutoka kampuni ya kutengeneza magari makubwa ya GF iliyoko Kibaha mkoani Pwani.

Kiwanda cha GF kina miaka mitatu tangu kianze kufanya kazi nchini na kina wafanyakazi zaidi ya 300 ambao wanachangiwa WCF.

Akbarali alisema alifika katika banda la WCF kupata uelewa zaidi kuhusu huduma zitolewazo na WCF ingawa kampuni yake tayari ilijisajili kwa mataka ya kisheria.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke mkoani Dar es Salaam ambaye ni mwajiri wa watumishi wa umma katika manispaa hiyo, Elihuruma Mabelya, alisema Temeke inao wafanyakazi zaidi ya 5,600 na ina idadi kubwa ya viwanda vikiwamo vikubwa na vidogo, hivyo WCF ni mdau muhimu kwao.

"WCF kwetu kama Temeke imekuwa kama mkombozi, kwa sababu wafanyakazi wanapopatwa na ajali au matatizo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao, mfuko unakuja kusaidia na hivyo kutoathiri uzalishaji mali unaoendelea ndani ya wilaya yetu," alisema.

Aliipongeza WCF kutokana na kuchukua jukumu la kumwinua mwananchi ambaye ni mfanyakazi na mwisho wa siku kuinua uchumi wa halmashauri na Taifa kwa ujumla.

Dofrian Junwalji kutoka Taasisi ya Trias Tanzania inayowawezesha wajasiriamali, alisema elimu aliyoipata katika banda la WCF imemwezesha kupata uelewa zaidi na ametambua umuhimu wa WCF kiuchumi kwa mwajiri na mwajiriwa.

"Mfanyakazi anapoumia maana yake atakuwa hazalishi. Kwa hiyo, WCF inabeba jukumu la kumwezesha kujikimu kimaisha kwa kumlipa fidia. Hivyo, mzunguko wa fedha unakuwapo, ataendelea kupata mahitaji yake kama vile chakula, kulipia pango na mahitaji mengine," alisema Junwalji.

Alitaja manufaa mengine kuwa ni pale mwajiriwa anapokumbwa na matatizo ya kuumia au kuugua WCF inampa huduma na hivyo mwajiri anabaki akiendelea na shughuli zake za uzalishaji na ikibidi mfuko unamlipa fidia ya gharama alizoingia mwajiri kumpa huduma mfanyakazi wake.

"Ningependa kuwashauri waajiri kujisajili na mfuko kwani kwa kufanya hivyo, matokeo ya uamuzi wa kufanya hivyo yatakuja kuonekana baadaye na uchangiaji wenyewe ni asilimia 0.5 tu ya mshahara wa mwajiriwa," alishauri.

Akitoa tathmini yake baada ya kutembelea banda la WCF na kujionea jinsi waajiri na wafanyakazi wanavyopatiwa huduma, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, alisema WCF inafanya kazi nzuri licha ya kuwa na muda mfupi tangu kuanzishwa kwake.

"Ninampongeza sana Mkurugenzi Mkuu, Dk. (John) Mduma pamoja na Bodi ya Wadhamini, wanafanya kazi kubwa na nzuri na ya mfano kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati," alisema.

Katika eneo la utoaji huduma, alisema zaidi ya asilimia 80 ya huduma zote za WCF zinatolewa kwa njia ya TEHAMA.

"WCF ina watu wenye weledi wa kutosha lakini niwahakikishie waajiri na wafanyakazi kuwa ustahimilivu wa mfuko huu ni wa uhakika hata kama itatokea 2050 mfuko haujafanya chochote unao uwezo wa kuwapa huduma wateja wake," alisema. Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. Mduma, aliwahakikishia waajiri na wafanyakazi kwamba mfuko uko imara katika kunatekeleza wajibu wake wa kulipa fidia stahiki na kwa wakati endapo mfanyakazi ataumia, kuugua au kufariki dunia kutokana na kazi.

"Tunayafanya haya ili kuhakikisha wawekezaji waliopo sasa na wanaokuja, wakute nguvukazi ya Tanzania ikiwa salama, na wale watakaopatwa na madhara yatokanayo na kazi, WCF itatumika kuwalipa fidia zao stahiki, kuwalipia matibabu yao ili kuhakikisha wanarejea kazini haraka iwezekanavyo," alisema.

## Chalamila asifu teknolojia zilizowasilishwa Sabasaba

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema teknolojia zilizowasilishwa katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) zitasambazwa nchi nzima.

Chalamila aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipotembelea maonesho hayo jijini Dar es Salaam na kusema zimeonyeshwa teknolojia nzuri ambazo zinatakiwa kufahamika.

Alisema kwa sasa wapo katika ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia kikubwa walichokishuhudia katika maonesho hayo yamebeba teknolojia mbalimbali ikiwamo sekta za kilimo na habari.

"Teknolojia hii imeweza kutumika kwa kiasi kikubwa na imekuwa ni pendezesho kubwa katika maonesho haya na kwa sasa baada ya teknolojia hiyo kuonekana kilichosalia ni kuisambaza iweze kufanya kazi katika nchi yetu ya Tanzania," alisema Chalamila.

Chalamila alisema anamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi, kwa ushirikiano wao mkubwa walioufanya wa kuhakikisha ushirikiano wa kidiplomasia umekuwa dhana muhimu katika maonesho hayo.

"Nimepita katika baadhi ya mabanda nimeona bidhaa zimebaki chache hiyo ina maanisha hawakuja kutazama bali ilikuwa ni maonesho ya watu kuja kununua bidhaa ambazo zimeletwa hapa kutoka kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi," alisema Chalamila.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), Latifa Khamis, alimshukuru Chalamila kwa kufanya ziara katika mabanda hayo na usimamizi katika kipindi chote cha maandalizi.

Alisema usalama na ulinzi umeimarika na wananchi wamefurahi kwa ujio wake wameona namna ambavyo serikali inaunga mkono katika maonyesho hayo.

# ZEEA yasaini mkataba wa kimkakati na TanTrade

**Na Beatrice Shayo**

WAKALA wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA), umesaini mkataba wa kimkakati na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade) kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali upatikanaji wa masoko endelevu ndani na nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kusaini makubaliano hayo Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Ali Suleiman Ameir, wakati wa Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayofanyika viwanja vya Mwalimu Nyerere, alisema wameona ni muhimu kuingia katika makubaliano hayo ya pamoja na TanTrade ili kuhakikisha soko la uhakika kwa wajasiriamali.

Alisema ZEEA wamepewa majukumu ya kuwasimamia wajasiriamali ili kuwapatia mitaji na masoko, kuwapa mafunzo ya kijasiriamali na kuanzisha programu za ujasiriamali.

"Kuwapatia masoko endelevu ili biashara zao ziwe endelevu na kumnyanyua mjasiriamali kuwa na kiwanda na awe mfanyabiashara mkubwa ili kuongeza pato la taifa," alisema Ameir.

Ameir alisema mkataba huo utaenda kumkomboa mjasiriamali na kuhakikisha bidhaa zao zinakwenda kuuzwa soko la ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema amempongeza Rais Mwinyi kwa kudumisha Muungano na kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya biashara ili kuwapa nguvu ya pamoja ya kuhakikisha taasisi zao zinasimama na kutoa huduma nzuri.

"Makubaliano tuliyoingia itasaidia kurahisisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi na mawakala watapata fursa ya kusoma," alisema.

Alisema wanategemea mambo mengi yatatokea na kuimarisha maeneo yenye changamoto kwa umoja wao utasaidia kutatua matatizo ya wajasiriamali ikiwamo kwenye upatikanaji wa masoko.

Aidha, alisema upatikanaji wa alama ya ubora awali ilikuwa ni kati ya Sh. 70,000 na Sh. 900,000 kutokana na bidhaa husika na kwa sasa inapatikana kwa Sh. 50,000 imepungua kwa asilimia 95.



# Kijiji chakosa majisafi miaka 48, wakazi waugua magonjwa

**Na Godfrey Mushi,**
ARUMERU

ADHA ya kukosa maji ya bomba kwa miaka 48 katika Kijiji cha Karangai, kilichoko Kata ya Kikwe, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, imesababisha baadhi ya wakazi wake kuugua na kulazwa hospitalini kutokana na tishio la magonjwa kama vile amoeba, kichocho, typhoid na kuhara.

Wananchi hao, hasa wanaoishi Kitongoji cha Miembeni, hawana huduma hiyo ya majisafi na salama tangu mwaka 1975, kwa sasa wanahemea maji machafu yanayotiririka kutoka kwenye mashamba ya mpunga ya Manyata.

Jana, Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji cha Miembeni, Parmena Kaaya, akizungumzia tatizo hilo alisema: "Ni kweli kwenye kitongoji changu wako kinamama ambao wamelazwa na watoto hospitalini, kwa sababu ya magonjwa ya amoeba na kichocho.

"Hivyo, tunaomba hii kero ya maji, serikali ituangalie kwa jicho la tatu, kwa sababu na sisi tuna haki ya kupata huduma hii kama Watanzania wengine."

Mkazi wa kijiji hicho, Hamisi Tajiri Alli, alisema wanazo taarifa kwamba kata yao ya Kikwe ilipata mgawo wa Sh. milioni 200 kwa ajili ya huduma ya majisafi lakini mradi huo haukufika Karangai.

"Tulipata taarifa kwamba kata yetu imepokea shilingi milioni 200, kwa ajili ya maji lakini mradi huo umeishia Maweni, na mpaka sasa hivi katika Kijiji cha Karangai na hasa Miembeni tunataabika kwa kukosa maji.

"Maji ambayo wananchi wanakunywa ni machafu na kibaya zaidi hatuna msemaji wa kutusemea, kwa sababu viongozi wetu kila mwaka wamekuwa wakituahidi na kutugeuza mtaji wa kura, wakati uchaguzi unapofika.

Zaidi aliongeza: "Mpaka hapa tunapoongea kuna wananchi wengi wako hospitalini wakitafuta tiba kutokana na kunywa maji machafu na wengine wameshafariki kwa ajili ya magonjwa yanatokana na kunywa maji machafu. Haya maji mnayoyaona yanatoka kwenye mashamba ya watu ya mpunga kutoka Usa River yanapotiririka kuja huku ndio wakazi wa Karangai ndio wanayatumia kwa ajili ya kunywa."

Aidha, Athuman Kitomari, mkazi mwingine wa Kijiji cha Karangai, alisema: "Maji ndiyo yanasababisha watu wanapata magonjwa ya matumbo kama kuhara, kipindupindu na typhoid. Sisi watu wa Karangai tunakunywa maji machafu, maji yanayotumika kunywa ni maji ya umwagiliaji na siyo maji yanayofaa kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

"Lakini cha kusikitisha kabisa, maji yametoka Bomang'ombe kule Rundugai, Wilaya ya Hai yamepita Kijiji cha Karangai kwenda Jiji la Arusha, lakini sisi hatuna maji.

...Maji yamepita kwenye ardhi yetu lakini tumekosa maji ya kunywa. Vijana walijitolea nguvu kazi, waliambiwa wajitolee kuchimba mitaro na wameishia kupoteza nguvu zao maji yameenda kwingine na hii siyo mara ya kwanza."

Wakati, Zaituni Masanja, alisema kijiji hicho cha Karangai kimetengwa na maendeleo, kwa kuwa serikali imewaacha waendelee kutumia maji yanayotoka kwenye mashamba ya mpunga ya Manyata.

"Kiukweli tuna adha kubwa na tunaathirika sana na magonjwa hasa kinamama na watoto kwa miaka mingi. Magonjwa tishio hapa Karangai kutokana na matumizi ya maji machafu tunayokunywa ni kichocho, typhoid na kuhara kwa sababu maji si salama.

Naye, Bertha Saimon, alisema kinamama na watoto katika kijiji hicho, wanapata shida ya kuchota maji kwenye mitaro inayotoka kwenye mashamba ya mpunga, ambayo ni hatari kutokana na tope na kuchafuliwa na mifugo, kinyesi.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kutokana na malalamiko hayo, Shabiu Waziri, Meneja Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), alisema:

"Ni kweli huduma ya maji katika Kijiji cha Karangai, Kata ya Kikwe, hayajafika kwenye vitongoji vyote ila yameishia Kitongoji cha Bondeni.

"Mpango wa serikali kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2023/24 ni kuusogeza Mradi wa Maji kutoka Bondeni kadi Miembeni ambako wananchi hawana hiyo huduma ya maji.

Ni matarajio yetu hadi kufikia Septemba mwaka huu kitongoji hicho kitakuwa kimefikiwa na huduma ya maji."



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel (mwenye shati jeupe), akipokewa na wakazi wa Kijiji cha Nakweni, Kata ya Shambarai, mkoani Manyara, alipofika kuwakabidhi zahanati iliyojengwa na Taasisi ya All for his Glory jana. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera (wa pili kushoto) na Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka. **PICHA: GIFT THADEY**

# Makandarasi waagizwa kukamilisha kazi kwa wakati

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, ameagiza makandarasi watatu waliopewa zabuni ya kutekeleza mradi wa maji wa Sh. bilioni 7. 282, kukamilisha kazi hiyo kwa mujibu wa mkataba.

Miradi inayotekelezwa na fedha hizo ni minne, ambayo inatekelezwa maeneo manne na inatarajiwa kunufaisha zaidi ya watu 54,000.

Mahundi, alitoa agizo hilo jana jijini Arusha, wakati wa halfa ya utiaji saini mikataba minne ya ujenzi wa miradi ya maji vijijini.

Miradi hiyo ni ile iliyoko Kata ya Uwiro na Kijiji cha Engatukoit, Wilaya ya Arumeru yenye thamani ya Sh. bilioni 1.877.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, Mkandarasi anayetekeleza mradi huo ni M/s Gopa Contractors Tanzania Limited, na wa pili ni ukarabati wa mradi wa maji vijiji vya Endonyawet na Matala, ulioko Wilaya ya Karatu, ambao una thamani ya Sh. milioni 839.618 na unatekelezwa na Mkandarasi M/s Climax Unit Limited.

Mradi mwingine ni uboreshaji wa maji Pori Tengefu la Poloreti wilayani Ngorongoro katika vijiji vya Ngobereti, Oloipir, Soitsambu, Losoito, Arash, Loswash, Kirtali, Mondoros, Sukenya, Orokanda na Olaika wenye thamani ya Sh.bilioni 3.553 ,ambapo kampuni ya M/s Jandu Plumbers Limited itatekeleza.

Alitaja mradi wa nne ni wa ushauri wa kitaalam kwa ajili ya usanifu wa miradi ya maji kwa Wilaya ya Arumeru, Monduli, Karatu na Longido wenye thamani ya Sh.bilioni 1.011 kutoka kampuni ya M/s Bene Consult (T) Ltd.

Alisema miradi hiyo ni lazima ikamilike kwa wakati na serikali inaimani katika kutumia wazawa, kufanikisha hatua mbalimbali za miradi ya maji husussan ya vipuri.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema serikali inafanya mambo mbalimbali ya kuleta maendeleo mkoani Arusha na kusimamia zaidi maslahi mapana ya Watanzania.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Joseph Makaidi, alisema miradi mitatu ni ya ujenzi wa miundombinu na mradi mmoja ni wa mtaalamu mshauri Bene Consult (T) Ltd

Aidha, Mkandarasi Mshauri wa Kampuni ya Bene Consult (T) LTD, Bernard Msaday, aliishukuru serikali kwa kuwaamini na kuahidi kuifanya kadri ya utaalamu wao ulivyo.

# Serikali yashauriwa kuwekeza masomo ya sayansi shuleni

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

SERIKALI imeombwa kutilia mkazo uwekezaji wa miundombinu na vifaa vya masomo ya sayansi katika shule zake za msingi na sekondari, ili kuwavutia wanafunzi waweze kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri wenyewe.

Ombi hilo lilitolewa jana na wazazi wa wanafunzi kutoka kata za Wilaya ya Tanga wakati wa maonyesho ya tatu ya masomo ya sayansi yaliyoandaliwa na wanafunzi wa madarasa ya awali, msingi na sekondari wa Shule ya Burhani iliyopo jijini humo.

Baadhi ya wananchi, akiwamo Mohamed Jumbe, Mkazi wa Ngamiani, alisema kutokana na ukweli kwamba nafasi za ajira ni zinahitajika jitihada za kutia msukumo katika masomo ya sayansi ili waweze kujiajiri wenyewe.

"Tumeshuhudia katika maonyesho haya wanafunzi wa darasa la tano wameweza kutengeneza sabuni, batiki, kuchapisha fulana, kutengeneza taa za majumbani, wamebuni mashine za kutolea uchafu na kuendesha shughuli kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kompyuta.

Hii yote ni kwa sababu wamesoma sayansi, kwa nini serikali isipunguze wimbi la ukosefu wa ajira, kwa kuwekeza kwenye masomo ya sayansi?"alihoji Jumbe.

Bushra Salehe, anayesoma kidato cha nne katika shule hiyo, alisema kupitia masomo ya sayansi anayofundishwa shuleni hapo, ameweza kujifunza kuchanganya tindikali tofauti na kutengeneza sabuni, mafuta ya kupakaa, batiki na kuchapisha maandishi na picha za aina yoyote na hivyo kumpa ujasiri wa kujiajiri na kuwaajiri vijana wenzake.

Mjumbe wa Bodi ya Shule hiyo, Mustapher Zavel, alisema Burhan imeanza mkakati wa kuisaidia serikali kupunguza wimbi la vijana kutegemea kuajiriwa kwa kufundisha sayansi, hususani mbinu za kuwasaidia kutengeneza bidhaa zinazopatikana katika mazingira yanayowazunguka.

Alipoulizwa kuhusu mkakati huo, Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Lusajo Gwakisa, alisema serikali imeanza kuwekeza katika masomo ya sayansi kwa kujenga maabara na vifaa vyake kwenye shule zote ili kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa vitendo.





# Mwenge wa Uhuru kukagua miradi ya bil.21/- Mwanza

**Na Vitus Audax**, MWANZA

MWENGE wa Uhuru umekagua na kuzindua miradi ya Sh. bilioni 21 katika Halmashauri za Mkoa wa Mwanza.

Akipokea Mwenge huo jana, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alisema kuwa katika mkoa huo Mwenge wa Uhuru unatarajiwa kukagua miradi 51 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 21.

Alisema pia unatarajiwa kuweka mawe ya msingi kwenye miradi 17 yenye thamani ya Sh.bilioni 13.7, kufungua miradi tisa ya zaidi ya Sh.bilioni 3.5, kuzindua miradi 15 ya Sh.bilioni 3.1 na kutembelea miradi 10 yenye thamani ya Sh.milioni 609.2. Makalla alisema kwa mwaka 2022 Mwenge wa Uhuru ulitembelea miradi 52 yenye thamani ya Sh. bilioni 18.7 na kwamba kwa mwaka 2023 Mwenge huo utatembelea miradi mitano iliyowekewa mawe ya msingi mwaka jana kwa ajili ya kuifungua.

Aidha, kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu, Abdalla Shaib Kaim aliiomba serikali mkoani hapa kumpa ushirikiano kwa Mkoa wa Mwanza hususani usahihi wa taarifa za miradi na nyaraka ili kufanikisha mbio za Mwenge huo kwa mwaka 2023.

Mwenge huo umekabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Hassan Bomboko kwa ajili ya kuukimbiza kwenye miradi sita ya wilaya hiyo kwa siku ya kwanza ikifuatia Manispaa ya Ilemela huku kauli mbiu ya mbio hizo ikiwa ni "Tunza mazingira, okoa vyanzo vya maji kwa ustawi wa viumbe hai kwa uchumi wa taifa."




Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2023, Abdalla Shaib Kaim (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Halfan Haule, baada kuweka jiwe la msingi la zahanati ya Kijiji cha Kurwaki, Musoma Vijijini mkoani Mara mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukosefu dawa, malalamiko ya wagonjwa vyamkera Ummy

**Na Alex Sayi,** MASWA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu amezitaka halmashauri kuhakikisha wanashughulikia upatikanaji wa dawa na kudhibiti hali ya wagonjwa kulalamikia juu ya ukosefu wa dawa.

Amesema kwa sasa tayari serikali imeongeza bajeti katika Bohari ya Dawa (MSD) ya usambazaji dawa nchini.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akihitimisha ziara yake mkoani Simiyu aliyoifanya katika Wilaya ya Maswa. Alisema kuwa katika halmashauri hiyo pekee serikali imeongeza fedha za dawa kutoka Sh. milioni 244 katika bajeti ya mwaka 2022/2023 hadi Sh.bilioni moja, huku bajeti ya dawa kwa Mkoa wa Simiyu ikiwa ni zaidi ya Sh.bilioni tano.

Aidha, aliwataka watumishi wa afya kuhakikisha wanatumia vyema uboreshaji wa miundombinu, dawa, vifaa tiba na vitendanishi uliofanywa na serikali kwa kutoa huduma bora na kuzingatia maadili ya kazi yao.

"Toeni huduma bora na siyo bora huduma, zingatieni weledi wa utoaji wa huduma ikiwa ni pamoja na maadili, miiko ya kitabibu, miongozo na sheria za serikali ili wagonjwa wasitumie muda mrefu kupata huduma, pia epukeni kutoa lugha chafu kwa wagonjwa," alisema Waziri Ummy. Aidha, aliwapongeza wahudumu hao kwa kupunguza vifo vya watoto na wajawazito kutoka asilimia 67 ya vifo vya watoto wachanga hadi asilimia 18 kwa mwaka 2023 huku kifo cha mama mjamzito kikirekodiwa kimoja kati ya wanawake 100 wanaojifungua wilayani humo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahya Nawanda, alisema kuwa mkoa huo umepokea zaidi ya Sh. bilioni 2.9 kwa ajili ya kuboresha miundombinu kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali. Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, alisema kuwa wilaya hiyo ina wafanyakazi wa idara ya afya 321, huku ikiwa na upungufu wa watumishi 505 sawa asilimia 61 kwa kada zote. Alisema watumishi 17 wameripoti kazini kati ya watumishi 46 waliotakiwa mwaka 2023 na kuiomba serikali kuendelea kuwaongezea watumishi lengo likiwa ni kuongeza ufanisi katika utoaji huduma.

Aidha, Addela Budima ambaye ni muuguzi wa Hospitali ya Wilaya ya Maswa alitoa ombi kwa Waziri Ummy juu ya kurudisha huduma ya bima toto ili kuwasaidia watoto wenye walemavu pamoja na wale wanaoishi kwenye mazingira magumu, wanaotoka katika familia maskini ili waweze kupata huduma bora.

## Waandishi wa habari wapewa jukumu kufichua ukatili

**Shabani Njia Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya Shinyanga, Johari Samizi, amewataka waandishi wa habari kuandika na kuibua vitendo vya ukatili vinavyofanyika katika jamii, ili serikali iweze kuchukua hatua za kisheria na kuwaokoa waathirika wa vitendo hivyo kwa wakati.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua semina ya siku mbili ya waandishi wa habari waliopo katika Mtandao wa Waandishi wa Habari za Ukatili wa Kijinsia Tanzania (TAJOGEV).

Alisema kuwa vitendo vya ukatili vimekuwa vikifanyika lakini elimu kwa jamii ya kuripoti vitendo hivyo bado ipo chini, hivyo ni jukumu la waandishi wa habari kutoa elimu na kuibua vitendo hivyo ili waathirika wapate msaada.

Naye Mwenyekiti wa Mtandao huo, Stella Ibengwe, alisema kuwa mafunzo hayo yanatolewa katika awamu ya kwanza kwa waandishi zaidi ya 40 kutoka katika mikoa 10, lengo likiwa ni kuwa na wanachama 500 katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Katika hatua nyingine Samizi alitembelea na kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule saba za msingi za halmashauri hiyo kupitia fedha za boost, kuagiza kasi ya ujenzi wake kuongezwa hadi kufikia Julai 19, 2023 viwe vimekamilika.

Alisema ameona hatua ya ujenzi wa vyumba hivyo na kuagiza kasi iongezeke ili ifikapo Julai 19 madarasa yote yawe yameshakamilika kujengwa na yajengwe kwa ubora na kiwango kinachotakiwa, ili kuboresha mazingira mazuri ya wanafunzi kusoma.

"Nimeona maendeleo ya ujenzi wa vyumba hivi vya madarasa kupitia fedha za boost naomba kasi iongezwe na ikifika Julai 19 madarasa yote yawe yamekamilika kujengwa," alisema Samizi.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Simon Berege, alitaja sababu ya kuchelewa kukamilika kwa wakati ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa kuwa kuchelewa kupatikana kwa malighafi ikiwamo saruji na mabati.

Alisema kwa sasa malighafi zote zipo na kasi itaongezeka na hadi kufikia Julai 19 vyumba vyote vya madarasa vitakuwa vimeshakamilika, huku akibainisha kuwa ujenzi huo umeshafia asilimia 90.




Ukurasa 13

Watanzania tunakitesa si kukienzi Kiswahili



**DP WORLD NI ZAIDI YA TICTS**

**Si kuongeza ufanisi ila kufumua uendeshaji 'kienyeji' wa bandari ili kupata tija, maendeleo**

Ukurasa 12


# BUFE

IJUMAA JULAI 14, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


# Umri wa kuishi Mtanzania waongezeka huku idadi ya vijana ikipaa maradufu

## • Lakini idadi kubwa ni 'jobless'
## •UNFPA yataka uwekezaji ajira

**Na Sabato Kasika**

MAKADIRIO ya ukomo wa umri wa kuishi kwa Watanzania yameongezeka hadi kufikia miaka 67 na miezi mitatu mwaka jana. Aidha, yanatazamiwa kufikia miaka 74 ifikapo 2035 na hilo litakuwa ni ongezeko la miaka saba na miezi miwili ndani ya miaka 12 ijayo.

Ripoti ya Makadirio ya Taifa ya Idadi ya Watu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaeleza kuwa kati ya mwaka 2013 hadi mwaka 2022, wanaume waliongeza umri wa kuishi kwa miaka minne na miezi sita, wakati wanawake waliongeza miaka mitano na miezi minne, wakiwazidi wanaume kwa miezi minane.

Hata hivyo, asilimia 60 ya Watanzania ni vijana wenye umri wa miaka 24 na idadi ya vijana hao inaendelea kuongezeka.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) zinazotolewa kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Watu Duniani huko Tunguu Zanzibar.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, Bryan Mark Schneiner, anasema zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania wana umri chini ya miaka 24 na kwamba idadi ya vijana inaongezeka, akifafanua kuwa ukuaji huo unamaanisha kuwa uwekezaji wa haraka katika ajira unahitajika.

"Uwekezaji katika ajira kwa vijana, mafunzo ya ufundi stadi, programu za kukuza ujuzi, vitasaidia kuwawezesha kuendesha maisha yao na kuchangia katika malengo ya maendeleo ya taifa," anasema Schneiner.

Mwakilishi Mkazi anafafanua kuwa ongezeko la umri linachangiwa na maendeleo katika sekta ya afya ambayo pia yamechochea ongezeko la watu na kwamba kwa mafanikio hayo, kuna haja pia kuwekeza kwenye ajira, ili vijana wawe na kazi.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (wa pili kulia), akiwa na baadhi ya mawaziri wakipata maelezo kutoka kwa Meneja Mawasiliano wa UNFPA, Warren Bright (aliyeshika meza), walipotembelea banda la shirika hilo katika maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani. Kushoto ni Mwakilishi Mkaazi wa UNFPA, Mark Bryan Schreiner. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**



Mwakilishi Mkaazi wa UNFPA Tanzania, Mark Bryan Schreiner, akihutubia katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani.

Ananukuu ripoti ya sensa ya watu na makazi ya 2022 inasema idadi ya watu nchini ni karibu milioni 62, ukuaji wake ni asilimia 3.2 ikimaanisha kuwa katika kila watu 100 wanaongezeka 30 kila mwaka, ambacho ni kiashiria kuwa uwekezaji kwa vijana hauna mbadala.

Anakumbusha kuwa kila Dola moja ya Marekani imewekezwa kwenye uzazi wa mpango, lengo likiwa ni kuboresha afya.

Anasema UNFPA itaendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine kuhamasisha suala la kupata ajira na afya bora hasa kwa wanawake, wasichana na vijana lakini kujua haki zao na kufanya maamuzi yatakayowawezesha kutimiza ndoto zao.

"Tunaipongeza serikali kwa dhamira yake ya kuendeleza rasilimali watu kupitia mikakati mbalimbali ya kuwekeza kwenye kusaidia vijana kupata ajira na kuboresha huduma za afya, ukuzaji ujuzi na usawa wa kijinsia na elimu," anasema.

**UKOSEFU WA KAZI**

Ukosefu wa ajira kwa vijana nchini, umeendelea kuwapo, na serikali imechukua hatua mbalimbali zikiwamo kuanzisha programu ya kuwahusisha vijana kwenye kilimo BBT, inayoendelea Bihawana mkoani Dodoma, ikitekelezwa na Wizara ya Kilimo.

BBT inawapa vijana mafunzo, ardhi na mitaji na kuzalisha mazao mbalimbali katika juhudi za kupunguza idadi ya wakosa kazi.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati anasilisha makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/2024 bungeni Dodoma hivi karibuni.

analiambia bunge kuwa viwango vya ukosefu wa ajira kwa vijana bado viko juu na kwamba vinahitaji juhudi zaidi ambazo zitasaidia angalau kuvipunguza.

Waziri Nchemba anakariri utafiti wa nguvukazi wa mwaka 2020/21 kuwa ukosefu wa ajira nchini kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 35 umekuwa ikiongezeka kutoka asilimia 12.1 kwa mwaka 2014 hadi asilimia 12.6 kwa mwaka 2020/2017.

"Tatizo hili la ukosefu wa ajira ni kubwa zaidi hasa kwa vijana wanawake ambao ni asilimia 16.7 ikiwa ni mara mbili ya kiwango kwa vijana wa kiume ambao ni asilimia 8.3," anaeleza Dk. Nchemba.

Anaeleza kuwa kiwango cha ukosefu wa kazi kinaendelea kushughulikiwa na juhudi mbalimbali zinazofanywa ikiwamo uanagenzi ingawa viwango vya ukosefu wa ajira bado ni vya juu na vinahitaji juhudi zaidi kuvipunguza.

Inaendelea Uk 12

## BIASHARA

DP WORLD NI ZAIDI YA TICTS

# Si kuongeza ufanisi ila kufumua uendeshaji 'kienyeji' wa bandari ili kupata tija, maendeleo

• Ni mkombozi wa SGR inapokamilika iunufaishe ukanda wote wa Maziwa Makuu usio na bahari

**Na Nimi Mweta**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amepata baraka za Kamati Kuu ya CCM kwenye mradi wa kukodisha uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, ambao baadhi ya wadau wanachanganya na umiliki wa miundombinu hiyo. Suala hilo limekuwa mwiba kwa CCM kwani limetoa agenda mpya kwa vyama vya upinzani, wengine wanataka maboresho ya hapa na pale lakini si kukaribisha uwekezaji wa uendeshaji.

Ni suala la kimkakati ambalo linatazamiwa kuendelea endapo kila eneo la uendeshaji litaandikiwa mkataba na ufikishwe bungeni ili kuridhiwa.

Labda kukwepa hali hiyo itabidi vyombo vinavyosimamia kuanzia wizara ya uchukuzi, ya sheria na katiba hata mamlaka ya usimamizi wa bandari zikusanye mikataba yote na kuitungia sheria, kuongezea mabadiliko madogo ya sheria ya bandari ili mikataba hiyo iwe viambatanishi vya uendeshaji. Kila eneo likiletwa kama mkataba mwingine itakuwa vigumu bunge kufanya kazi, kwani wadau watajipanga na 'mizinga' ya marekebisho, wakati bunge kimsingi limeridhika na kuridhia mkataba wa awali kati ya Tanzania na Ufalme wa Dubai.

DP World ni waendeshaji, watakaokabidhiwa ofisi. Kinachoshangaza ni kutafuta ni kwa sababu gani mkataba huu umekuwa mfupa mgumu kwa makundi tofauti ya watu, siyo wadau kwa maana ya wale wenye maslahi na 'bandari huru' kama ilivyo sasa, kwa maana kuwa wana uwezo wa kuiendesha wanavyotaka.

Kwa mfano mzigo ukitoka China lazima ukabidhiwe kwa mdau wa bandari ya Dar, ukifika ushushwe, upelekwe bandari kavu na kote huko yako makaratasi ya kujazwa, na kulipiwa. DP World



Bandari 'mama' ya Dar es Salaam inayotegemewa na nchi za Maziwa Makuu.

inabadili hali hiyo, kwa kufuta ngazi hizo tofauti na kukomesha ulaji.

Bado kutakuwa na nafasi ya uwakala kwa mfano ulipiaji wa mizigo kwani kodi zitaendelea kukusanywa na Mamlaka ya Mapato (TRA), pamoja na shughuli nyingine ambazo hazifafanuliwi kwa kina, za ulinzi na usalama. Baadhi ya wahusika, kama Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, wanasema ujio wa DP World hauna tofauti na TICTS, ambayo ilikuwa imeshika baadhi ya magati na kreni kupakuwa mizigo kutoka kwenye meli.

Kwa kusema hivyo alikuwa anaainisha kuwa tulishazoea, wakati mkataba ulilazimishwa. TICTS ilipata mkataba wa miaka mitano kipindi cha kwanza cha uongozi wa Rais Benjamin Mkapa, na mwezi mmoja kabla ya uchaguzi mkuu mwaka 2005 ukapelekwa bungeni muswada wa kuongeza muda kwa miaka 15.

Ndiyo TICTS ilipofanikiwa kusimamia baadhi ya magati ya meli kushusha mizigo kwa miaka 20, kwani wadau waliwekwa pembeni. Safari hii hali ni tofauti kwani mkataba unaopelekwa DP World ni mpana zaidi, halafu ni makubaliano ya kitaifa na siyo zabuni tu ya uwekezaji iliyotangazwa na wizara, Mamlaka ya Bandari, halafu DP World ishinde ni tofauti kabisa.

Ingekuwa ni tenda imetolewa na DP World ikashinda, ingefanya kazi chini ya Mamlaka ya Bandari kama 'mwajiri' wake, kama ilivyo kwa makandarasi wa Wakala wa Barabara, TANROADS. Mkataba wa DP World ni wa ngazi nyingine, unaoashiria kuwa wanafanya maamuzi ya kiuendeshaji kuhusu meli na mizigo kwa jumla. Kampuni hiyo itasimamia pia ajira katika shughuli zilizochini yake na kwa njia hiyo wadau wanakuwa na wasiwasi kama watabakia.

Katika ufafanuzi wake, Waziri Mbarawa, ametoa picha ya uwezekano wa ajira nyingi kuongezeka, lakini ufanisi katika dunia ya sasa ni kutumia teknolojia na hasa ya habari na mawasiliano. Tayari kuna mashine za aina tofauti za kuinua vitu na kuvipanga viwandani, na kwa vile waajiriwa na wasimamizi wao ndiyo wanaoshutumiwa siyo tu kwa ucheleweshaji wa kupakua mizigo ila hata kwa upotevu wa mali, kunyofoa vifaa au viongezeo vya magari, si rahisi kuona DP World ikiwatumia. Kubadili mfumo ni kuweka ATM bandarini, hivyo mzigo unakuja mtu anabonyeza kitufe unatoka.

Ziko ahadi nyingine za Waziri Mbarawa ambazo ni rahisi kuzitilia shaka, kwa mfano maelezoo kuwa hadi kufikia mwaka 2032 (miaka tisa kutoka sasa) asilimia 60 ya bajeti ya serikali itatokana na mapato bandarini. Si rahisi kuona takwimu hiyo imepikwa vipi na kwa mpangilio gani iwe ni wa ufanisi bandarini au ufanisi wa uchumi kwa jumla.

Kuna uwiano kati ya viwango au idadi ya ajira za watu na mapato, hivyo bandari haiwezi kuajiri mamia kadhaa ya watu kusimamia mitambo ya kupakua na kuondoa mizigo halafu ichukuwe nafasi ya sekta kadhaa kwa pamoja.

Kinachoweza kufanikishwa zaidi na ujio wa DP World ni matumizi ya reli ya kisasa ya SGR itakapoanza majira kama haya mwakani. Pale bandari yote ya Dar es Salaam itakapokuwa chini ya DP World kwa upande wa mizigo, usalama wake na ufikishaji wake, nchi za ukanda wa Maziwa Makuu zisizo na bahari zitaitumia Dar es Salaam kwa urahisi zaidi.

Wanauamini mfumo wa utendaji wa DP World na siyo kukubali tu uhakikisho wa Mamlaka ya Bandari, kwani kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Serikali (PIC), Jerry Silaa, kuwa waendeshaji hao hawana jipya, na hawawezi kubadilika hivi karibuni.

Kwa maana hiyo SGR ikianza kazi na inategemea zaidi mizigo ya hapa nchini haitaweza kufikia ufanisi wa uwezo wake wa kusafirisha shehena. Na hitaji hilo halitasahihishwa kwa kuweka watendaji wenye kisomo cha juu au 'wakali' bandarini.

Ni suala la uwakala wa kampuni yenye mtandao mkubwa na hivyo uwezo wa kuchukua shehena kokote duniani na kuikabidhi kwa muagizaji katika 'bandari'ya mwisho, hata kama ni kilomita milioni kutoka bandari ya mwisho, kwa mfano Kigali nchini Rwanda au Ndola Zambia.

Mfumo wa hivi sasa ni kupandisha na kushusha shehena kwa kutumia mamlaka au mawakala tofauti, iwe ni wa meli, bandari au forodha, ambao ni wazi wanawekwa pembeni 'kama wote' ili DP World ifikishe shehena kwa wateja.

Kimsingi DP World ni uendelezaji wa kazi iliyokuwa inafanywa na TICTS ila kwa upana zaidi, kwani inachukua maeneo karibu yote ya kupakua shehena hasa kwa kuingiza kutoka nchi za mbali, nje ya majahazi yanayotoka Unguja au Comoro.

Wakati TICTS ilikuwa ni suala la ufanisi wa bandari kwa kutegemea sekta binafsi kwa kiwango kikubwa, bila kuingiza mashakani Mamlaka ya Bandari katika kazi yenyewe ya upakuaji mizigo, DP World ni hatua nyingine.

Ni kuhoji ufanisi na uwezo wa kiutendaji wa mamlaka hiyo, na kutumia mtandao wa uchukuzi (logistics) ambao unatumiwa na kampuni hiyo, mfumo wa mawasiliano na vyomho vya usafirishaji au mifumo ya uwajibikaji kiutendaji ambayo haiwezi kujengwa na TPA kwa sasa.

Kubwa zaidi ni kuhakikisha kuwa SGR itatumika ipasavyo wakati au kipindi ikianza kazi, na kwa njia hiyo kuleta ufanisi zaidi kiuwekezaji pale ambapo wingi wa shehena zinazopelekwa kwa reli utawezesha bei, gharama za kutumia huduma hizo kuwa za chini kiasi kwa majirani wanaotegemea Tanzania kusafirisha.

Nje ya kutumia kwa njia hiyo, kurudisha mikopo iliyokopwa kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo itabidi gharama za kuitumia ziwe kubwa, watuamji wa nje wawe wamepungua na muda si mrefu kiwango cha ulipaji madeni cha bajeti ya taifa kitakuwa hakibebeki kirahisi.

Ni hapo nchi itaingia katika maandamano kudai kupunguzwa bei za mafuta, au kutopanda nauli za daladala, ufanisi utakuwa mdogo bandarini na SGR iwe ni mzigo ambao uhitaji wake ni mdogo kikanda.



Reli ya kisasa ya SGR ikikamilika inaweza kuwa na tija zaidi iwapo bandari zitakuwa zinafanyakazi kwa ufanisi na teknolojia ya kisasa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

## Umri wa kuishi Mtanzania waongezeka huku idadi ya vijana ikipaa maradufu

**INATOKA UK. 11**

**MBINU CHAFU**

Licha ya ukosefu wa ajira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, anasema baadhi ya vijana wanaosaka ajira wamekuwa wadanganyifu kwa lengo la kujipatia kazi zinazotangazwa na serikali.

Anasema serikali ilitangaza nafasi za ajira na kuahidi kuwapa kipaumbele wenye mahitaji maalum.

Hata hivyo, anafafanua kuwa walijitokeza vijana 171,916 katika kada ya ualimu na afya kupitia TAMISEMI, waombaji 1,169 walijitambulisha kuwa wanaishi na ulemavu, lakini uchunguzi ulibaini kuwa zaidi ya waombaji 419 hawakuwa na ulemavu wowote.

Anafafanua, akisema kati ya 64 waliosema wanaishi na ualbino ni 24 pekee waliosema kweli huku 40 wakidanganya.

Hata hivyo, anasema kati ya waombaji waliojitokeza ni 18,449 pekee walipata nafasi na kupangiwa vituo vya kazi baada ya kukidhi vigezo vya kitaaluma na taratibu za uombaji.

"Waliochaguliwa na kupangiwa vituo vya kazi katika kada ya afya ni 5,319 na ualimu ni 13,130 na kati yao wenye mahitaji maalum ni 111 sawa na asilimia 0.84," anasema Angellah.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Watanzania tunakitesa si kukienzi Kiswahili






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

TANGU itangazwe kuwa kila Julai 7 ni Siku ya Kiswahili Duniani, ni miaka mwili sasa Watanzania tunatoka kifua mbele, kujivunia lugha hiyo tukitilia maanani kuwa hapa ndipo lilipo chimbuko lake.

Lugha hii inatuheshimisha sana duniani, lakini nadhani bado tumejisahau na kujifungia ndani na kuona kama ni jambo la kawaida tu, ituheshimishe isituheshimishe tunachukulia poa, bora matumbo yanajaa.

Kwa mwaka huu, hivi karibuni wataalamu mbalimbali wa Kiswahili wakiwamo wanahabari waandamizi, wakapiga kambi Zanzibar wakajadili mengi hasa jinsi ya kukiendeleza na kukienzi.

Wanahabari hatimaye, wakarejea sehemu zao za kazi nikiamini kutakuwa na mabadiliko miongoni mwao katika matumizi ya maneno na misamiati ya Kiswahili kwenye vyombo vyao, hususan watangazaji, lakini wapi!

Nikaamini katika kile ambacho husemwa, kuwa ni maadhimisho tu na sherehe, na baada ya hapo mambo hurejea kama kawaida. Kwamba siku ya maadhimisho utasikia kauli na miito mbalimbali ya viongozi.

Mikutano inaandaliwa viongozi wanapanda majukwaani kuhutubia kuenzi jambo kwa nguvu, lakini inapofika jioni ya kuzama jua, watu wanalala na wanapoamka asubuhi jua limechomoza kila kitu ni kipya. Yaliyopita si ndwele.

Hivi kweli Watanzania tumedhamiria kukienzi na kukilinda Kiswahili kama tunavyosema? Inakuwaje mpaka sasa tunaendelea kulumbana kuhusu Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia?

Tunatamba kuwa duniani kote sasa Kiswahili kinafundishwa, tunasikia mpaka Urusi Kiswahili sasa kitaanza kufundishwa shuleni, lakini sisi tunalumbana kuhusu kitumike au kisitumike kufundishia.

Juzi tu hapa nasikiliza redio, kuna kipindi cha watoto kinaitwa Watoto Show si kiitwe Kipindi cha Watoto, mtangazaji anaitwa Aunt na si shangazi tuna vituo vya redio na luninga vinaitwa majina ya kigeni lukuki kulikoni.

Tuna taasisi nyingi na biashara zenye zina majina ya Kiingereza kwanini tusiyape ya Kiswahili, ukienda barabarani kuna kampuni za mabasi zote ni Kizungu kwenye ndege ipo Air Tanzania, kwani haiwezi kuitwa 'Ndege wa Tanzania? La sivyo basi tuzipe majina kama bundi, mwewe, kunguru na tai. Ukiambiwa unasafiri na bundi inakuwa uchuro na hiyo ni kutokana na imani za kishirikina kuwa anahusika na vifo vya wagonjwa anapotua nyumba wanapouguliwa.

Mathalan, katika kutangaza wanyama na raslimali zetu, kwa nini kampuni za usafiri kam 'Best Trans' zisiitwe fisi au mbwa mwitu, mbweha au nguchiro? Ili mradi majina yawe yanakitangaza Kiswahili.

Angalia hata vyama vya siasa, walioweza ni CCM na CHADEMA wengine utasikia CUF, NCCR-Mageuzi na ACT-Wazalendo. Tutakifikisha mbali Kiswahili kweli?

Ukienda kwenye muziki ndiko kabisaa, muziki unaoimbwa ni wa Kiswanglish au Kiswakinge, Kiswazulu, Kiswausa. Wasanii wetu tunaowapa kipaumbele leo, na kuwaita magwiji wa muziki wa Tanzania, wanaimba Kiswahili wakichanganya na Kiingereza, Kizulu (Amapiano) na Kihausa!

Kama kweli tunaamini sisi ndio magwiji wa Kiswahili na tunaotegemewa na dunia kukieneza na kukifundisha basi tuache kuitana 'dokta' badala ya 'daktari', 'injinia' badala ya 'mhandisi'.

Tatizo lipo kwa tuliowapa dhamana ya kusimamia jambo hili, kwani hata wao ama hawakijui vizuri Kiswahili au hawakipendi na pengine hawataki hata watoto wao wakijue na ndiyo sababu wanawasomesha kama si nje basi kwenye shule zao hizi za kigeni-akademi!

Tukiacha masuala ya 'ayam sore' na 'oh mai Godi' na hasa tunapokuwa tayari tumeweka moja baridi moja moto kichwani, bila shaka tutakiheshimu, kukipenda na kukikumbatia Kiswahili na kudhihirisha umahiri na ubingwa wetu katika kukiendeleza.

Vinginevyo, kila mwaka tutaandaa matamasha na kufanya rejea za nchi zinazotangaza na kufundisha Kiswahili duniani, lakini taratibu tukirudi nyuma na kupoteza ugalacha wetu katika lugha hiyo adhimu.

Kumbukeni titi la mama li tamu ingawa la mbwa, na tusiache mbacha wetu kwa msala upitao, kwa kuamini tu kuwa lugha za Wazungu ni tamu kuliko maziwa yatokayo kwenye titi la mama.

Majirani watatuacha kwenye mataa tukikodoa macho na kutupora heshima tuliyojijengea duniani kwa muda mrefu. Tusitumie Kiswahili kama tunavyoambiwa eti ni fursa ya ajira, bali tujifunze tukijue ndipo tukafundishe kwingineko.

**Alamsiki!**

UCHUMI

## STEVEN SHADRACK KANGERO

# Mzawa aliyeamua kuhamishia uwekezaji mikononi mwa wananchi wilaya aliyozaliwa

**Na Mwandishi Wetu, MWANGA**




WAWEKEZAJI wengi wanajijengea vitega uchumi kama shule, zahanati na benki na kuvimiliki. Lakini wapo wachache wanaovijenga na kuvifanya mali ya umma ili vimilikiwe na kila mmoja kwenye kijiji au kata.

Mmoja wa wafanyabiashara wanaokumbukwa kwa kufanya hayo ni Steven Kangero wa Mwanga mkoani Kilimanjaro, anayeacha alama ya kujenga shule za umma, nyumba za walimu pamoja na miundombinu ya huduma kwa ajili ya wananchi wa wilaya ya Mwanga na kuwaachia umiliki kamili.

Ni mzaliwa wa wilaya hiyo, ambaye pamoja uwekezaji binafsi kwenye mifugo, mashamba, ushauri wa kiuchumi na fedha, wadau wanaofuatilia juhudi binafsi za kupambana na umaskini na kufufua uchumi wa Tanzania kuanzia miaka ya 1970 hadi sasa watamkumbuka Kangero.

Watalihusisha jina lake na kazi kubwa ya kuboresha maisha ya wakulima maskini vijijini, upanuzi wa vitega uchumi kitaifa na kuboresha mifumo ya fedha kwenye jamii zisizokuwa na benki.

ANAPOWEKA ALAMA

Anaanza kufanya mambo kuanzia miaka ya 1970, akisaidia kujenga himaya kubwa ya wakulima wa pamba Kanda ya Ziwa alipofanikisha kuwafikishia matrekta. Ndiye anayekusanya fedha kutoka kwa wakulima vijijini, anazilinda na kuzipeleka kwa kampuni ya magari jijini Dar es Salaam na kuwapatia pembejeo hiyo muhimu, anasema Andrew Chenge, Mwanaseheria Mkuu wa Serikali mstaafu.

Ni mzaliwa wa Bariadi, aliyekuwa anazungumzia mchango wa Kangero kwenye maendeleo ya nchi, wakati wa kumuaga na mazishi ya mfanyabiashara huyo aliyewekeza kitaifa na ndani ya jamii anayotoka.

Anasema:“Wakati anasaidia wakulima kupata matrekta hakukuwa na benki alitembea na maelfu ya fedha za wakulima wa pamba mfukoni kisha akarejea na kumkabidhi kila mmoja trekta lake. Alikuwa mwaminifu kupindukia.”

Ni wakati wa kuelezea kazi kubwa ya ujenzi wa taifa alioufanya Kangero wakati wa uhai wake, kijijini kwao Kiruru Wilaya ya Mwanga Julai 1, 2023 wakati wa mazishi ya mfanyabiashara aliyeitwa “shujaa wa wilaya ya Mwanga.’

Alikuwa mwaminifu, mwadilifu na mfanyabiashara aliyetengeneza mtandao wa maendeleo kwa Tanzania na hata leo nyumbani kwake Mwanga na hata Bariadi wanafurahia mafanikio yaliyotokana na imani, bidii na juhudi zake, anamsifu, Chenge mbunge mstaafu wa Bariadi.

Mbunge wa Mwanga (CCM), Joseph Tadayo, anamtaja Kangero kuwa ni mwekezaji aliyekuwa karibu na nyumbani kwake-Wilaya ya Mwanga na mkoa wa Kilimanjaro pia.

“Kwenye elimu jina lake lipo amejenga Sekondari ya Kata ya kwanza ndiyo Lembeni Sekondari, leo imeendelea zaidi hadi kidato cha sita ni Lembeni High School, ameijenga tena akishirikiana na mwenzake aliyewekeza kwenye usafiri na usafirishaji Ali Mbeserero walijenge nyumba ya mwalimu mkuu.”

“Hakupenda ndugu zake wa Mwanga wakose matibabu kwa sababu hiyo alishiriki bega kwa bega kujenga Kituo cha Afya cha kisasa cha Kisangara,” anasema na kuongeza kuwa ni mtu ambaye alitumia fedha, nguvu na muda wake kuwekeza katika kuhudumia watu wa nyumbani kwake na taifa.

**ANA ALAMA KITAIFA**

Tadayo anasema, kwa upande wa sekta binafsi ana mengi kitaifa na ameacha historia, akiwa mshiriki mkuu kutekeleza sera ya ubia baina ya sekta ya umma (serikali) na sekta binafsi-PPP.

“Kangero ameshirikiana na sekta ya umma kwenye mradi wa utafiti wa mafuta ukanda wa bahari, akifanikisha kupata wataalamu wa kampuni ya Dominion Oil, si hivyo tu, kwenye madini amehusika na kupatikana kampuni ya The ARL Gold, kutafiti dhahabu.”

“Katika ujenzi wa bwawa la umeme Kihansi, alishiriki katika kufanikisha upatikanaji wa kampuni ya Impregilo ya Italia iliyofanyakazi kubwa, “Tadayo anabainisha anapopewa jukwaa kumwelezea Kangero.

Kangero mara kwa mara alionyesha kujali maendeleo ya Mwanga na Tanzania pia, akinukuliwa akisema kuwa watu hawawezi kuendelea kuishi bila shule,vituo vya afya na hata benki ambazo wakulima na wafugaji wanaweza kuweka fedha zao na kupata mitaji au mikopo kwa ajili ya uwekezaji wao wenyewe, anakumbusha Waziri Mkuu Mstaafu, Cleopa Msuya.

Ili wananchi wa Mwanga waweze kujiinua kiuchumi, wakulima, wafugaji na wanakijiji waweze kujitegemea, ilianzishwa Mwanga Community Bank-Benki yaWanajamii wa Mwanga ambayo Kangero ilikuwa mdau mkubwa wa uanzishwaji wake, anasema Waziri Mkuu huyo wa zamani.

Benki hiyo imekua zaidi na sasa imebadilika na kuitwa Mwanga Hakika Bank, akipanuka na kuwa wanahisa na matawi mengi.

Msuya aliyekuwa pia mbunge wa Mwanga, anapozungumzia juhudi za Kangero anaongeza kuwa;

Anawaambia watu kuwa, Kangero ameleta mafanikio makubwa katika kubadilisha maisha ya watu na kufanikisha kupatikana hali bora na endelevu kwa wengi katika ngazi ya mtu mmoja, jamii pia taifa, mambo yanayobaki kuwa muhimu sana kwa sekta zote na wananchi wenzake wa Mwanga.

Itakumbukwa kuwa wilaya ya Mwanga ni miongoni mwa wilaya chache nchini Tanzania zilizokuwa na benki za wana jamii ambayo Kangero alishiriki kuianzisha katika harakati zake za kusaidia kuboresha sekta ya fedha ikiwa ni njia ya kufanikisha mageuzi ya kiuchumi yaliyoanza miaka ya 1980.

Kangero ni nguli wa uwekezaji kitaifa na kimataifa, kwa mujibu wa Msuya, akisema alipenda pia wana jamii na nyumbani kwake kuhusike na uwekezaji, akianzisha mashamba ya kufuga kuku wanaouzwa katika masoko ya Ulaya.

Anamwelezea kuwa kwa ujumla amewahusisha karibu wote, watu wa nyumbani, lakini pia kujenga ushirikiano kati ya watu wa nyumbani na familia ya Mwanga, serikali na jumuiya ya kimataifa ya wafanyabiashara kwenye soko la nje likiwamo la Ulaya.

Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini (CCM), FeliX Mrema, anasema ni mwekezaji ambaye ameshiriki kuleta maendeleo sehemu nyingi ikiwamo Arusha, alikokuwa anashirikiana naye kuwasaida wananchi wake kutatua kero mbalimbali.

Anaheshimika pia kwa ushirikiano na mataifa jirani hasa Kenya, anasema Naomi Namsi Shabaan, mwanasiasa kutoka jimbo la Taveta, ambaye ni mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kuwakilisha jimbo hilo mwaka 2002 kwa tikiti ya KANU.

Anasema mafanikio yake kisiasa na kibiashara yanamhusisha Kangero, alimshauri na kumsaidia katika masuala mengi.





Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telak (katikati), akizungumza na kinamama wanaoendelea na matibabu ya fistula ya uzazi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi-Sokoine, alipotembelea jana, kuona jinsi utoaji wa matibabu ya ugonjwa huo unavyoendeshwa na Hospitali ya CCBRT ya Dar es Salam kwa kushirikiana na hospitali hiyo na kampuni ya Equinor Tanzania. Wengine ni Meneja wa Miradi wa CCBRT, Yohana Kasawala (kushoto), bingwa wa magonjwa ya kinamama kutoka CCBRT, Dk. James Chapa (kulia) na (wa pili kulia) ni Dk. Naomi Makota wa Equinor. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Marais 15 Afrika kushiriki Jukwaa la Chakula

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema marais wa nchi 15 za Afrika wamealikwa katika Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF 2023), huku akiwataka Watanzania kuchangamkia fursa zitakazotokana na jukwaa hilo.

Akizungumza jana kwenye kikao cha maandalizi ya jukwaa hilo lilipangwa kufanyika kati ya Septemba 5 hadi 8 mwaka huu jijini Dar es Salaam, Ulega alisema ni muhimu wadau wa sekta ya mifugo na uvuvi kushiriki kwa wingi kwa kuwa kongamano hilo ni fursa kwao.

"Tunataka kila atakayekuja Tanzania asiondoke bila kutuachia faida, sisi wafugaji na wavuvi tuwe kipaumbele wakati wa kupata heshima ndio huu, tunataka muwe kimbelembele wa maendeleo kwenye mkutano huo, hatutaki muwe wanyonge na hapaswi mdau yeyote abaki nyuma," alisema.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina uwezo wa kuchangia katika mabadiliko ya mfumo mzima wa chakula kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi.

"Wizara imeazimia kuboresha na kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi kwa nia ya kulisha Afrika na dunia, kama mnavyoelewa mifugo na uvuvi ni jibu kwa usalama wa chakula, lishe, uchumi na ajira," alisema.

Alisisitiza jukwaa hilo ni fursa adhimu ya kujifunza kutoka nchi zingine, fursa za kukutana na wadau wa teknolojia mbalimbali, uwekezaji wa aina tofauti, kuingia ubia na taasisi kubwa na kazi na masoko.

"Naomba kutoa rai kwenu ya kushiriki bila kukosa katika kongamano hilo la kihistoria kuhusu mifumo ya chakula barani Afrika, pia hakikisheni mnashiriki kwa wingi na kuhakikisha kuwa fursa na mafanikio ya sekta za mifugo na uvuvi nchini yanafahamika duniani kote," alisema.

Kadhalika, Ulega alisema wizara hiyo imeweka mikakati mikubwa katika kuongeza mchango wake kwa pato la taifa kutoka asilimia 6.7 mwaka 2022/23 hadi kufikia kwa asilimia 10 kwa mifugo na kutoka asilimia 1.8 hadi asilimia tatu kwa uvuvi.

Alisema pamoja na mchango huo kwa sekta hizo bado kuna mahitaji makubwa ya mazao ya mifugo na uvuvi katika soko la ndani na nje ya nchi.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula, alisema ni lazima Watanzania watafute thamani ya Tanzania kwa kuwa na mpango mkakati yenye tija na kuwa na takwimu halisi na zenye ushahidi.

Awali, akitoa salamu za wadau wa mifugo, Hamoud Salim aliahidi wadau hao watatumia ipasavyo fursa hiyo kupitia maonesho ya bidhaa bora zinazozalishwa nchini.

# RC aja na mkakati kudhibiti utoro kwa wanafunzi

**Na Augusta Njoji,** KONDOA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amebainisha mkakati wa kudhibiti tatizo la utoro kwa wanafunzi katika Wilaya ya Kondoa na kuagiza hatua zichukuliwe kwa wazazi wanaofumbua tatizo hilo.

Senyamule aliyasema hayo jana wilayani humo katika kikao cha Baraza la Madiwani cha kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22.

"Suala la elimu ni agenda ya kudumu ni lazima watoto waende shule na muwataje wote wanaotoroka na kuwachukulia hatua wazazi wasiopelekea watoto shule. Kila Ijumaa tuwe tunapata taarifa za watoto kwa watendaji wa kijiji na kata wana Kondoa tulivalie njuga suala hili," alisema.

Aliwataka wazazi kutambua umuhimu wa watoto wao kupata elimu na kutofumbia tabia ya utoro.

Aidha, alihimiza halmashauri hiyo kudumisha ushirikiano baina ya madiwani na watendaji ili kuendelea kuwa na hati safi.

Alisisitiza halmashauri kuweka mkazo mkubwa kujibu hoja zote za ukaguzi na maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LAAC) ili kuondokana na mrundikano wa hoja nyingi zisizofanyiwa kazi.

Alisema: "Kamati ya Fedha ya Madiwani inatakiwa kukutana kila mwezi kuwa na ajenda ya kudumu ya kujadili mwenendo wa ujibuji wa hoja za ukaguzi na kuchukua hatua stahiki pale inapobainika kuwa menejimenti imefanya uzembe katika kufanyia kazi hoja za ukaguzi".

# Kamati ya Siasa CCM yampa maagizo Mkurugenzi Manispaa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Singida imemtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe kutosita kuwachukulia hatua watumishi wanaojihusisha na matumizi mabaya ya fedha na usimamizi duni wa miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa CCM wilayani humo, Lucia Mwiru, alitoa agizo hilo jana baada ya kamati hiyo kukagua miradi ya ujenzi wa shule inayoendelea kujengwa kupitia fedha za mradi wa Boost.

"Mkurugenzi wa miradi ya Boost katika imejengwa vizuri sana lakini kama wapo watumishi ambao kwa namna moja ama nyingine wamejihusisha na ufujaji wa fedha na usimamizi mbovu wachukulie hatua," alisema.

Alimtaka mkurugenzi huyo kukaa na wataalamu ili kurekebisha kasoro zilizobainika katika baadhi ya miradi michache afya na ya elimu ili kukamilika na wananchi kunufaika nayo.

Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, akizungumzia ziara hiyo alisema utaratibu ambao unaboresha utendaji kazi wa watumishi katika halmashauri ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mbunge wa Singida Mjini, Musa Sima, alipongeza walimu kwa usimamizi mzuri wa miradi ya Boost na ile ya serikali na kuwaasa watekelezaji wengine wa miradi inayoendelea na itakayokuja kuiga mfano mzuri wa walimu katika kusimamia miradi.

# DASPA yatambulisha mbegu mkombozi kwa wakulima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Wakulima la Uzalishaji Mbegu Dodoma (DASPA), limetambulisha aina tano za mbegu za karanga na mtama kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo zitakazokuwa na tija kwa wakulima.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mtendaji Mkuu wa DASPA, Aithan Chaula, alisema mbegu hizo zimefanyiwa utafiti na Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu nchini (TOSCI) pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mbegu Tanzania (TARI).

Alizitaja mbegu hizo kuwa ni nari nut 2015, Naliendele 2016 na nachi 2015 ambazo ni za karanga, wakati mbegu za mtama ni TARI SORI 2 na mmacia ambazo hutoa mazao mengi.

"Mbegu hizo ni bora sana hivyo wakulima wajiandae kuzitumia ili wafanye kilimo chenye tija ambacho kitaleta matokeo chanya, ikiwemo kuwasaidia wao na familia," alisema Chaula.

Alisema matumizi ya mbegu bora yatasaidia sana wakulima hasa wa vijijini kupata mazao mengi kutokana na mbegu bora zilizofanyiwa utafiti na mamlaka husika.

Alifafanua kuwa mtama una fursa kubwa ya kuzalishwa kwa wingi zaidi kama zao la chakula kuziba nafasi ya mazao mengine ambayo yameathiriwa na ukame kutokana na na mabadiliko ya tabia nchi.

Naye, mkulima Glads Ngalawa alisema kumekuwa na tatizo kubwa ya ndege kushambulia mazao, akashauri wakulima wakapewa mbinu za kuzuia mazao kushambuliwa na ndege ikiwamo mtama.





Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mabonde, Kata ya Kalobe, jijini Mbeya jana, alipofanya ziara ya kukagua shughuli za maendeleo hasa ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mwalimu awalaza wanafunzi darasani, RC atoa maagizo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera amemwagiza Ofisa Elimu wa Mkoa huo kumchukulia hatua za kinidhamu mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Loleza, Sabina Haule kwa tuhuma za kuwalaza wanafunzi darasani kama sehemu ya adhabu.

Homera alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kushtukiza shuleni hapo kwa lengo la kufuatilia jambo hilo ambapo alisema kitendo cha mwalimu huyo kuwalaza wanafunzi darasani ilipitiliza kutokana na hali ya hewa ya Mbeya kwa sasa.

Alisema mwalimu huyo aliwalaza darasani wanafunzi hao 70 wanaosoma tahasusi ya HGL (Historia, Jiografia na Lugha) wakati hali ya joto ikiwa imeshuka mpaka kufikia nyuzi joto tisa hali ambayo ilikuwa inahatarisha afya za wanafunzi hao.

Homera alisema mwalimu huyo aliwalazimisha wanafunzi hao kulala darasani bila vifaa vya kujifunika na akafunga bweni lao na kuondoka na funguo.

"Hawa watoto baadhi wanaweza wakawa na magonjwa kama vile pumu, vifua na magonjwa mengine ambayo hayataki baridi, sasa wewe unawalaza darasani unataka wakifa hiyo kashfa aipate nani? Namwagiza ofisa elimu amchukulie hatua mwalimu huyu," alisema Homera.

Alisema baadhi ya wanafunzi hao wanaweza wakawa na shida zingine ikiwamo kuwa katika kipindi cha hedhi na hivyo kitendo cha mwalimu huyo kufunga bweni kiliwanyima fursa ya kujisitiri.

Pamoja na agizo hilo pia alisema serikali haitawafumbia macho wanafunzi wote watukutu bali itawachukulia hatua ili iwe fundisho kwa wengine.

Mkuu wa Shule ya Loleza, Mwalimu Betseba Nsemwa, alisema walipopata taarifa hizo kutoka kwa wanafunzi waliwasikiliza na wakawaomba msamaha kwa adhabu hiyo ambayo ilikuwa imepitiliza.

Alikiri kuwa wapo baadhi ya wanafunzi ni watukutu na kwamba hivi karibuni walitwaita wazazi wao kwa ajili ya kuwashughulikia na wakalimaliza lakini adhabu iliyotolewa na mwalimu huyo ilikuwa imepitiliza.

"Niliongea na wanafunzi nikawasikiliza malalamiko yao na nikawaomba msamaha kwa adhabu waliyokuwa wamepewa, ni kweli wapo baadhi yao ni watundu lakini adhabu hiyo kweli ilizidi," alisema Mwalimu Betseba.

Awali akihojiwa na Mkuu wa Mkoa, Mwalimu Sabina, aliomba radhi kwa tukio hilo na kwamba yeye hakukusudia kuwalaza wanafunzi hao darasani isipokuwa waliamua wenyewe kulala kama sehemu ya kumkomoa.

Alisema yeye ndiye mwalimu anayesimamia mabweni na hivyo alibaini kuwa baadhi ya wanafunzi wa tahasusi hiyo ya HGL ni watukutu ndio maana akaamua kuwaadhibu.

Alisema wamekuwa wakitoroka madarasani na kwenda kujifungia mabwenini na kila akienda kuwafuatilia wanajificha kwenye vungu za vitanda ili wasionekane na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

"Mimi sikuwaambia walale darasani lakini yawezekana walifanya hivyo kwa lengo la kunikomoa mimi, naomba nisamehewe," alisema Mwalimu Sabina.

# Mke wa mbunge atoa msaada taulo za kike shuleni

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKE wa Mbunge wa Lupa, wilayani Chunya mkoani Mbeya, Veronica Masache ameendelea kuwasaidia wanafunzi wanaosoma katika shule mbalimbali wilayani Chunya kuhakikisha wanahudhuria shuleni siku zote za masoko kwa kuwagawia taulo za kike kwa ajili ya kujisitiri wanapokuwa kwenye siku za hedhi.

Aidha, ameendelea kugawa sare na vifaa mbalimbali vya shule kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wakiwemo wenye ulemavu na wanaotoka kwenye familia zenye uwezo duni.

Veronica amekuwa akigawa taulo hizo kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ambazo sio za kiserikali ikiwamo Taasisi ya DIDO Mwanafunzi Initiative.

Alianza kugawa taulo hizo jana ambapo aligawa vifaa vya shule kwa watoto wenye mahitaji maalumu wanaosoma katika Shule ya Msingi Kibaoni na taulo za kike kwa wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Sekondari, Amos Makalla na Itewe.

Alisema alianza kutoa misaada hiyo mwaka jana kwa lengo la kusaidia kupunguza utoro kwa watoto wa kike ambao wamekuwa wakitoroka wakati wanapokuwa kwenye kipindi cha hedhi kwa kukosa vifaa vya kujisitiri.

Alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha kushuka kwa kiwango cha ufaulu kwa watoto wa kike kutokana na kukosa masomo wakati wanapokuwa kwenye siku hizo.

"Lakini hawa watoto wenye ulemavu nimewanunulia sare na daftari ili na wao washiriki vizuri kwenye masomo, tumekuwa tukifanya hivyo kila mwaka kwa lengo la kuiunga mkono serikali kuboresha elimu," alisema Veronica.

Alisema ataendelea na utaratibu huo kila mwaka kwa kuhakikisha anashirikiana na mashirika mbalimbali kuyasaidia makundi hayo.

# Serikali yanunua MRI kusaidia wakazi Nyanda za Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini waliokuwa wanalazimika kusafiri kwenda katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kupata kipimo cha kiuchunguzi cha MRI, wameondokana na adha hiyo baada ya serikali kununua mashine kwa ajili ya Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Mashine hiyo ilizinduliwa juzi ili kuwarahisishia wananchi huduma za kiuchunguzi ambazo walikuwa wanazikosa na kulazimika kutumia gharama kubwa kwenda Muhimbili.

Mkuu wa Idara ya Radiolojia wa Hospitali hiyo, Dk. Cecilia Ngatunga, alisema mashine hiyo ni ya kisasa na ina uwezo wa kutambua magonjwa mbalimbali ambayo vipimo vingine haviyatambui. Alisema ina uwezo wa kutambua magonjwa kama saratani, uvimbe wa aina mbalimbali ndani ya mwili, mabadiliko yanayoendana na umri wa binadamu pamoja na mapungufu ambayo baadhi ya watu wanazaliwa nayo.

Alisema kipimo hicho kilikuwa hakipo kwenye hospitali hiyo na hivyo wagonjwa walikuwa wanalazimika kwenda katika maeneo mengine zikiwamo hospitali za watu binafsi.

"Mshine hii ni ya kisasa, katika kitengo chetu cha mionzi tulikuwa hatuna, tunaishukuru serikali kwa kuinunua hii mashine, itatusaidia kuwatibu wagonjwa hapa hapa badala ya kuwapatia rufani kwenda maeneo mengine," alisema Dk. Cecilia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema kipimo cha juu zaidi ambacho walikuwa nacho katika idara hiyo ni cha CT-Scan ambacho kilikuwa hakina uwezo wa kutambua baadhi ya magonjwa.

Alisema wagonjwa waliokuwa wanahitaji vipimo zaidi madaktari walikuwa wanalazimika kuwaandikia rufani kwenda Muhimbili jambo ambalo lilikuwa linawagharimu fedha nyingi kuliko endapo wangeipata mashine hiyo mapema.

"Kuanzia leo mashine hii ya kisasa imeanza kufanya kazi na sisi tuwahakikishie wananchi kwamba wataendelea kupata huduma bora katika hospitali yetu hii badala ya kwenda Muhimbili," alisema Dk. Mbwanji.

Akizindua huduma hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mkakati wa serikali ni kuendelea kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa maeneo yote hasa kwa kuwasogezea huduma muhimu.

Alisema kutokana na kuwapo kwa huduma hiyo katika hospitali hiyo ya kanda kutawavutia pia wananchi wa nchi jirani zikiwamo Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo pamoja na mataifa mengine.

Aliwataka wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuhakikisha wanajitokeza kupima afya zao ili wapate matibabu ya magonjwa mbalimbali yanayowakabili. Kuboreshwa kwa huduma za afya katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, kunatajwa kuwa kutasaidia nyingine kupunguza usumbufu kwa wagonjwa kufuata matibabu nje ya mikoa inayonufaika.

# TAMWA-Zanzibar kupigania huduma bora afya ya uzazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar), kimeahidi kuendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha wanawake na wasichana wanapata huduma bora za haki ya afya ya uzazi nchini.

Ofisa wa Tathmini na Ufuatiliaji wa TAMAWA-Zanzibar, Mohammed Khatib, alisema hayo katika kikao cha kupitia kitini cha mafunzo ya haki za afya ya uzazi kilichofanyika katika ofisi za chama hicho zilizopo Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema masuala ya afya ni muhimu kwa jamii lakini utafiti wa awali uliofanywa na TAMWA umebaini bado waandishi wa habari hawaripoti kwa kina masuala hayo hasa yanayohusiana na haki ya afya ya uzazi kwa wanawake na wasichana.

Hivyo, alisema TAMWA itawajengea uwezo waandishi wa habari ili kuwa wabobezi katika kuripoti masuala ya afya kwa wanawake na wasichana.

Aliwaomba wadau kutoa maoni ya kuboresha kitini hicho ambazo kitawasaidia wakufunzi kutoa elimu sahihi kwa waandishi wa habari na hatimaye kuwasaidia wanawake na wasichana kufurahia haki ya afya ya uzazi.

Akiwasilisha rasimu ya mwongozo huo, mkufunzi Juma Khamis Juma, alisema kitini hicho ni muhimu na kitakuwa mwongozo wa kufundishia masuala yanayohusiana na afya. Wakichangia katika kikao hicho, baadhi ya washiriki waliomba TAMWA kuuboresha mwongozo huo kwa kuainisha baadhi ya mada zitakazoangazia tatizo la saratani ya shingo ya kizazi na matiti ambayo inaathiri wanawake wengi.

Mwandishi Mwandamizi, Shifaa Said alisema miongozo mengi kuhusu SRHR inaweka kando maradhi hayo, badala yake inashughulikia zaidi masuala kama UKIMWI, uzazi wa mpango na maradhi ya kuambukiza.

Kikao hicho kiliandaliwa na TAMWA kwa kushirikiana na Wellspring Philanthropic Fund.



Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Migombani mjini Unguja juzi, wakati akitoa taarifa kuhusu katazo la wanaume kusuka nywele. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Taasisi za muungano zatakiwa kujipambanua kwa wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Khadija Khamis Rajab, amezitaka taasisi za muungano ambazo zinafanya kazi na wizara hiyo kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kuwajengea uwelewa juu ya kazi zao wanazozifanya.

Aliyasema hayo jana alipofanya ziara maalum ya kikazi katika Shirika la Posta Tanzania, Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) pamoja na Mamlaka ya Mawaliano Tanzania (TCRA).

Alisema kwamba wapo wananchi wengi pamoja na viongozi katika serikali hawana uwelewa mzuri juu ya shughuli zinazofanywa na taasisi hizo visiwani humo jambo linalosababisha kutokafahamika kwa huduma wanazozitoa.

Akizungumzia juu ya Shirika la Posta Tanzania alisema pamoja na mabadiliko na maendeleo ya teknolojia bado shirika hilo lina kazi kubwa za kufanya jambo litakalosaidia kuingizia mapato ya serikalini.

Pia, alisema ipo haja ya kufanya kikao cha pamoja na taasisi nyingine za serikali ili kuangalia namna nzuri ya kushirikiana na kuingizia mapato serikali.

Akiwa katika ofisi za TTCL Katibu Mkuu huyo aliwataka viongozi na watendaji hao kuendelea kutoa ushirikiano ili kufanikisha dhamira njema ya kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia mawasiliano yaliokuwa bora.

Akiwa katika ofisi za TCRA Zanzibar, alipokea taarifa kutoka kwa Meneja wa TCRA ofisi hiyo, Esuvatie Masinga.

# Wawekezaji watakiwa kukata bima ya majanga

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wawekezaji kukata bima ili kuwasaidia wakati wanapopatwa na majanga.

Aliyasema hayo wakati alipofanya ziara eneo la Paje Mkoa wa Kusini Unguja kukagua hoteli tano za kitalii zilizoungua katika kijiji hicho mwanzoni mwa wiki hii.

Makamu huyo aliwaahidi wawekezaji wa hoteli hizo kwamba huduma zote stahiki na muhimu katika eneo hilo zitarejea kwa haraka iwezekanavyo.

Alisema licha ya kutokea kwa majanga hayo ya moto lakini wawekezaji wanayo fursa ya kuendelea kuwekeza Zanzibar na ni visiwa vyenye amani na utulivu na serikali itatoa ushirikiano kwa wawekezaji.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa, aliwashukuru wananchi wa Kijiji cha Paje kwa umoja na ushirikiano walioonyesha kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha moto huo unadhibitiwa. Alisema kusambaa haraka kwa moto huo kumesababishwa na hoteli hizo kuwa karibu sana, hivyo aliwashauri wawekezeji kuzingatia suala la kuacha nafasi wakati wanapojenga.

Alisema hatua hiyo itasaidia athari kuwa ndogo wakati panapotokea majanga na pia itarahisisha gari ya zima moto na uokozi kufika kwa haraka katika eneo la tukio. Katika hatu nyingine, Hemed alifika eneo la Donge Mkoa wa Kaskazini Unguja kutoa pole kwa familia ya watoto wanne waliofariki mwanzoni mwa wiki hii baada ya kuzama katika shimo la kuchimba mchanga ambalo lilikuwa na maji.

Alisema serikali imepokea kwa masikitiko taarifa ya msiba huo na kuwaomba wanafamilia kuwa na subira.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuwa waangalifu na kujua mienendo na maeneo wanaocheza watoto wao ili kuepukana na majanga mbalimbali.

Akielezea kwa masikitiko kuhusu tukio hilo, Hassan Suleiman Khamis kwa niaba ya familia hiyo alisema kuwa watoto hao waliondoka nyumbani kwao wakielekea eneo la Kondeni kwa ajili ya kuvuna matikiti na ndipo umauti huo ulipowakuta.

Alisema kuwa baada ya kurudi Kondeni waliingia katika shimo hilo kwa lengo la kuoga, ndipo walipozama na kufariki dunia ambapo mtoto mmoja amelazwa hospitalini na hali yake inaendelea vizuri.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



Bwana **NELSON LEOPOLD RWECHUNGURA** amepoteza cheti chake cha kidato cha nne kilichotolewa mwaka 2018 Sekondari ya St Stephen Boys.Namba yake ni **S4740/0085.** Taarifa za kupotea kwa cheti zimefunguliwa kituo cha Polisi Dar es salaam na kupewa namba **DAR/URA/RB/224078/2023.** Atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ERICK ZAKARIA NYAMOHANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba **T944 AUP.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/235690/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NADINE MAHAMUDU JAHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **LIFO XY49-10** yenye usajili namba: **MC 582 CWQ,** CHASSIS NAMBA: LRYPCHL05J0011727 na ENGINE NAMBA: **1P52FMH18102516.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:**KAH/RB/TR/457/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......66/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: SHADRACK JOSEPH MABULA wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA: VICTORIA BENEDICT WAKULYAMBA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 20 Mwezi 07 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 12 mwezi 07 mwaka 2023

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP.117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL REGISTARION OF DOCUMENTS ACT, (CAP.117)**

**CHANGE OF NAME BY DEED POLL.**

**I, ISMAEL LOKAJI** a Tanzanian adult,male,Christian by faith resident of Sanawari ya Juu street,within Olturoto ward at Arusha,formely known as **ELIYA LOKAJI,**
**WITNESSS AND IT IS HEREBY DECLARED** as follows:-

1. That,I do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former name **ELIA LOKAJI** in lieu thereof I assume and adopt the name of **ISMAEL LOKAJI.**
2. That,in pursuance of such change of name as aforested I hereby declare that I shall at all time hereinafter in all Records,Deed and Instruction in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and you upon all occasions whatsoever use and sign the said name **ISMAEL LOKAJI** as my name in lieu of the said **ELIYA LOKAJI** renounced as aforesaid.
3. That **I HEREBY AUTHORISE AND REQUEST** all person to designate and address me in the name of **ISMAEL,LOKAJI.**

**I,ISMAEL LOKAJI** make this declaration conscientously believing the same to be true and accordance with the provisions of the Oaths (Judicial Proceedings and Statutory Declarations) Act,Cap.34 R.E 2019.
**IN WITNESS WHEREOF I** have here in to subscribed the name **ISMAEL LOKAJI** on the day and in the manner hereinafter appearing.

DEPONENT



BEFORE ME:-
Name: MITEGO, METHUSELA ROBERT
Signature
COMMISSIONER FOR OATHS

**NOTICE OF AN ORDINARY GENERAL MEETING**
**OF**
**CONTINUITY BUILDERS TANZANIA LIMITED**

**Notice of an Ordinary General Meeting made under Section 345 of the Companies Act,**

**No. 12 of 2002 of the Laws of United Republic of Tanzania; To the Members of the Company:**
**NOTICE IS HEREBY GIVEN** that an Ordinary General Meeting of the Members of the Company will be held on the 14th day of August 2023 from 10.00am at the Company Registered Offices to discuss the following Agenda;

**Ordinary Business;**
1.1. To adopt the agenda of the Meeting;
1.2. To lay before the members the accounts of the company showing how the winding-up of the Company has been conducted, and the properties of the Company have been disposed off and that the same was done accordingly.
1.3. To discuss any other business which may arise during the meeting. Dated on this 14th day of July 2023

.......................................................................

**MAGDALENA MANJALE (THE LIQUIDATOR)**
**PLOT NO 49, BLOCK II, HOUSE NO 26, CORRIDOR AREA, INGIRA ROAD, P.O. BOX 6267, ARUSHA TANZANIA**

**NOTICE OF AN ORDINARY GENERAL MEETING**
**OF**
**BULLET SAFARIS LIMITED**

**Notice of an Ordinary General Meeting made under Section 345 of the Companies Act,**

**No. 12 of 2002 of the Laws of United Republic of Tanzania; To the Members of the Company:**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** that an Ordinary General Meeting of the Members of the Company will be held on the 14th day of August 2023 from 10.00am at the Company Registered Offices to discuss the following Agenda;

**Ordinary Business;**
1.1. To adopt the agenda of the Meeting;
1.2. To lay before the members the accounts of the company showing how the winding-up of the Company has been conducted, and the properties of the Company have been disposed off and that the same was done accordingly.
1.3. To discuss any other business which may arise during the meeting. Dated on this 14th day of July 2023

.......................................................................

**MAGDALENA MANJALE (THE LIQUIDATOR)**
**PLOT NO 49, BLOCK II, HOUSE NO 26, CORRIDOR AREA, INGIRA ROAD, P.O. BOX 6267, ARUSHA TANZANIA**

**COMPANY NO. 154999477 ZAIQA LIMITED**
**P.O.BOX 2754,**
**ARUSHA-TANZANIA.**
**(UNDER VOLUNTARY WINDING UP)**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to all **CREDITORS and DEBTORS of ZAIQA LIMITED** and the **GENERAL PUBLIC** that **ZAIQA LIMITED** is undergoing Voluntary winding up under the appointed liquidator one **FREDRICK MUSIBA KATIMBA.**

All debtors of the company and all persons holding in their possession any assets/properties of the company to pay their debts to the liquidator at the address below not later than 12:00 noon the 4TH day of August 2023 and to surrender the assets and the said properties to the liquidator at the address below not later than 12:00 noon 4th day of August 2023. All creditors of the company are hereby given notice that they should submit their claims with supporting documents to the liquidator at the address below not later than 12:00 noon the 4th day of August 2023 without fail.

.......................................................................

**FREDRICK MUSIBA KATIMBA (LIQUIDATOR)**
**ARUSHA, DISCTRICT ARUSHA CBD, WARD KATI, STREET JACARANDA, JACARANDA BUILDING FIRST FLOOR, BLOCK L, PLOT 7, P.O.BOX 457.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 76 OF 2023**

**In the Matter of the Estate of the Late: JASTINI ANTANAMANA MANGI**

**By 1. NORAH JASTINI MANGI**
**2. ......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 27 day of 07/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**

**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Madai Na.31/2023**

**Jina la Mdai PAULO MAKARANGA NA WENZAKE(6)**
**Jina la Mdaiwa VITESSE COMPANY(T)LIMITED**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa VITESSE COMPANY(T)LIMITED**
**DAR ES SALAAM**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) **MADAI YA PESA SH 5,905,000/-ZA MAUZO YA PILIPILI NA FIDIA YA USUMBUFU.**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 17 Mwezi 07 Mwaka 2023 saa 2;30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa
kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 06 Mwezi 07 Mwaka 2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAIKA IRENEI NGOWI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 693 CEP – TOYOTA SUZUKI.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **WMB/RB/0619/2023.**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0745 700 710.

Nipashe MWANGA WA JAMII

# Maandamano ya siku tatu yanukia Kenya

**NAIROBI, Kenya**

KATIBU Mkuu wa Chama cha upinzani cha ODM nchini Kenya ambaye ni Seneta wa Jiji la Nairobi, Edwin Sifuna, ameitisha maandamano ya siku tatu kuanzia wiki ijayo.

Sifuna aliapa kuzidisha maandamano dhidi ya serikali hadi matakwa yao yatakapotekelezwa.

Kulingana na Sifuna, maandamano hayo ya siku tatu ya kila wiki yatafanyika kuanzia Jumatatu hadi Jumatano na yatakamilika tu wakati Rais William Ruto atakapokubali kupitia upya Sheria ya Fedha ya 2023 yenye utata.

"Kuanzia wiki ijayo, siku tatu mfululizo za maandamano, Jumatatu, Jumanne, Jumatano hadi William Ruto atakapoelewa kuwa watu wanateseka na kubatilisha sheria hii jinsi alivyoiweka juu yao," alisema.

Akizungumza katika kipindi cha runinga ya Citizen jana, alisema kwamba serikali inafaa kusikiliza matakwa ya Wakenya wengi kabla ya kuchukua suala hilo mikononi mwao.

"Ni afadhali wakati huu ambapo watu kama Sifuna, Raila, Osotsi, wanaongoza maandamano haya. Siku Wakenya watakaposhughulikia suala hili wenyewe hakutakuwa na mtu wa kuwaita kwenye meza," alisema.

Pia aliikemea serikali kwa kutangaza awali kuwa itawakamata viongozi wa Azimio wakidai kwamba hawatarudi nyuma katika vita vya dhidi ya serikali na wako tayari kukamatwa kwa sababu hiyo.

"Hakuna mtu atakayetutishia. Hakuna kitu ambacho hawa watu hawajasema. Hakuna wanachoweza kututisha nacho ikiwa ni kukamatwa tuko tayari," aliongeza kusema. **BBC**



Baadhi ya wakazi wakipita karibu na nyumba zilizobomoka kutokana na mapigano yanayoendelea nchini Sudan. **PICHA: AFP**

# Kaburi la halaiki lagundulika Darfur

**KHARTOUM, Sudan**

MAITI ya watu 87, miongoni mwao wa kabila la Masalitis wamezikwa katika kaburi la pamoja katika jimbo la Darfur magharibi mwa Sudan.

Taarifa hiyo ilitolewa na ofisi ya haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa ikisema kuwa inazo taarifa za kuaminika kwamba ni vikosi maalumu vya dharura (RSF) vinahusika na mauaji hayo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Umoja wa Mataifa, wakazi wa eneo hilo walilazimika kuitupa miili hiyo kwenye sehemu iliyo wazi.

Miili ya wanawake na watoto ilikuwa miongoni mwa maiti hizo.

Kadhia hiyo ilitokea kati ya tarehe 20 na 21 mwezi uliopita karibu na mji mkuu wa Darfur wa EL-Geneina.

Baadhi ya watu walifariki kutokana na majeraha ambayo hayakutibiwa baada ya wimbi la vurugu za vikosi vya dharura vya RSF na wanamgambo washirika, zilizotokea baada ya kuuawa kwa gavana wa eneo hilo.

Kamishna wa Haki za Binaadamu wa Umoja Mataifa, Volker Turk, amelaani vikali mauaji hayo.

**Kadhia hiyo ilitokea kati ya tarehe 20 na 21 mwezi uliopita karibu na mji mkuu wa Darfur wa EL-Geneina.**

# Majenerali waondolewa jeshini Russia

**MOSCOW, Russia**

JENERALI wa ngazi ya juu wa jeshi la Russia, amevuliwa wadhifa wake baada ya kuwaambia wakuu wa kijeshi ukweli kuhusu hali mbaya iliyopo katika mstari wa mbele.

Meja Jenerali Ivan Popov, alikuwa kamanda wa kikosi cha 58, ambacho kimekuwa kikipigana katika eneo la kusini la Zaporizhzhia nchini Ukraine.

Katika ujumbe wake wa sauti, Meja Jenerali Popov alisema aliuliza maswali juu ya kuwapo kwa kiwango cha juu cha majeruhi na ukosefu wa msaada wa silaha.

"Ilikuwa ni lazima niseme ilivyo, au ninyamaze na kukaa kuwa mwoga," alisema.

Aliongeza "Sikuwa na haki ya kusema uwongo kwa jina lako, kwa jina la wenzangu waliokufa mikononi, kwa hivyo nilielezea shida zote zilizopo."

Ujumbe huo wa sauti ulitumwa kwa telegram na Mbunge wa Urusi, Andrei Gurulyov, ambaye ni kamanda wa zamani wa kijeshi na mtoa maoni wa mara kwa mara kwenye TV ya serikali.

Hata hivyo, haijafahamika lini ujumbe huo ulirekodiwa.

Miongoni mwa masuala ambayo Meja Jenerali Popov alisema ni ukosefu wa mifumo ifaayo ya betri za kaunta kusaidia kuzima mashambulio ya vifaru vya Ukraine, pamoja na ukosefu wa ujasusi wa kijeshi.

Kamanda huyo aliasema kuachishwa kwake kazi kulipendekezwa na makamanda wakuu ambao aliwashutumu kwa uhaini na kuidhinishwa na waziri wa ulinzi wa ulinzi, Sergei Shoigu.

Aidha, Kamanda wa zamani wa Russia ambaye hajawahi kuonekana tangu uasi uliofanywa na kundi la Wagner, mwezi Juni inaelezwa yuko kwenye makazi yake anapumzika.

Andrei Kartapolov, mwenyekiti wa kamati ya ulinzi, alisema kwamba jenerali Sergei Surovikin alikuwa hapatikani na kuibua wasiwasi kuhusu mahali aliko, amepumzika.

Ripoti ambazo hazijathibitishwa zilieleza Jenerali Surovikin alizuiliwa kwa mahojiano kuhusu kuhusika kwake katika uasi huo. Alidaiwa kuwa na uhusiano wa karibu na mkuu wa Wagner Yevgeny Prigozhin.

Mamluki wa Wagner walijaribu jaribio la uasi tarehe 23 na 24 mwezi Juni walipotishia kuelekea Moscow.

Uasi huo ulisitishwa baada ya Rais wa Belarus Alexander Lukashenko kuingia makubaliano na Prigozhin.

Wapiganaji wa Wagner wametakiwa kujiunga na jeshi la Russia waende nyumbani au waende Belarus.

Jumatano wizara ya ulinzi ilisema kwamba kundi hilo lilikuwa likikamilisha mpango wa kutoa silaha na vifaa vingine vya kijeshi, ikiwamo vifaru 2000, vifaa vya kurushia roketi, bunduki za kukabiliana na ndege na silaha nyingine.

Jenerali Surovikin mara ya mwisho alionekana hadharani katika kanda ya video wakati wa uasi akiwataka wanajeshi wa Wagner kusitisha vitendo vyao.

Ripoti za vyombo vya habari baadaye zilisema alikuwa amekamatwa, lakini hakukuwa na uthibitisho rasmi ama tamko kuhusu aliko.

Jenerali huyo alikuwa akisimamia vikosi vya Russia nchini Ukraine mwezi Oktoba lakini akandolewa miezi mitatu. **BBC**

# MOALIN AAHIDI MAKUBWA KMC FC LIGI KUU 2023/2024

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa KMC FC, Abdulhamid Moalin, amesema kazi kubwa aliyonayo ni kukisuka upya kikosi chake ili kuanza msimu mpya kikiwa imara na chenye ushindani.

Moalin ametangazwa kuwa kocha mpya wa KMC akichukua mikoba iliyoachwa na Jamhuri Kihwelo 'Julio' ambaye alikinusuru kikosi hicho na janga la kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili baada ya utambulisho juzi jioni, Moalin alisema anashukuru kupata nafasi nyingine ya kufundisha soka hapa nchini kwa kuonyesha uwezo wake na kutowaangusha mashabiki wa timu hiyo.

Moalin alisema anatarajia kufanya kazi yake kwa weledi ni kuifanya KMC kuwa moja ya timu zitakazowania mataji katika msimu mpya.

"Nashukuru Mungu kwa kupata nafasi nyingine tena ya kuifundisha timu ya Tanzania, huu ni mtihani mkubwa kwangu kwenda kuifanya timu yenye kikosi imara, najua ligi kwa sasa nchini ni ngumu na hata msimu ujao haitokuwa rahisi, lakini nimekuja hapa na nimekubali nikijua haya yote," alisema kocha huyo wa zamani wa Azam FC.

Kuhusu atakavyokisuka kikosi chake, alisema anatengeneza kikosi ambacho si cha kuwa kusindikiza timu nyingine kama ilivyokuwa msimu iliyopita.

"Najua kwa sasa hiki walichokifanya viongozi wa KMC wanataka kuifanya klabu kuwa makini na mshindani wa kweli katika Ligi Kuu na soka la Tanzania, si msindikizaji tena, hivyo na mimi sasa nipo tayari kwa hili, nakwenda kutengeneza kikosi bora cha ushindani wa kweli wa ligi kwenye kuwania mataji," Moalin alisema.

Moalin alitimuliwa Azam FC Agosti mwaka jana baada ya kuhudumu kama Kocha Mkuu kuanzia Januari akirithi mikoba ya Mzambia, George Lwandamina.

KMC ilinusurika kushuka daraja baada ya kuifunga Mbeya City katika mechi za mtoano, ambayo pia ilikutana na kipigo cha jumla cha mabao 4-1 kutoka kwa Mashujaa FC ya Kigoma ambayo ilifanikiwa kupanda daraja.



Mwanzilishi wa wazo la Ubongo Kids, Cleng'a Ng'atingwa (kulia), akizungumza kuhusu maadhimisho ya miaka 10 ya Ubongo Kids yatakayofanyika hivi karibuni jijini, Dar es Salaam. Katikati mwanzilishi wa Kitengo cha Michoro, Rajabu Semtawa na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa taasisi hiyo, Imani Lipumba. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kiduku atamba kumchapa Apei

**Na Abdallah Mataka**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Twaha Kassim 'Kiduku', ametamba hatawaangusha mashabiki wake katika pambano la kuwania ubingwa wa WBF dhidi ya Godi Apei kutoka Afrika Kusini litakalofanyika Julai 29, mwaka huu jijini Mwanza, imeelezwa.

Kiduku alisema anaendelea vyema na mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha kuwapa burudani na heshima wadau wa mchezo huo wa hapa Tanzania.

Alisema lengo lake ni kuona anaendelea kutangaza vizuri kipaji chake katika kila pambano atakalopanda ulingoni na kuongeza kambi yake iko mkoani Morogoro.

"Sitawaangusha mashabiki wangu, naendelea vyema na maandalizi ili nipate ushindi katika pambano hili, tuungane pamoja kwa ajili ya kuiletea heshima nchi yetu," alisema bingwa huyo wa mkanda wa mabara wa UBO.

Naye Kocha wa Kiduku, Charles Ilanda, amesema bondia wake yupo tayari kwa ajili ya pambano hilo na amemtaka mpinzani wake kujiandaa kupokea kichapo.

"Tunatarajia atakuwa bondia mzuri kwa sababu hatujamwona akicheza, imekuwa vigumu kwetu kupata taarifa zake, lakini huwa tunafanya maandalizi kwa ajili kupambana na bondia wa aina yoyote ile," alisema kocha huyo.

Kiduku ambaye ni mwenyeji wa Morogoro, ameshinda mapambano 22 kati ya michezo 24 aliyopanga ulingoni.

## Mashujaa yasajili straika wa Mtibwa

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali inayoonyesha Mashujaa FC iliyopanda daraja msimu huu imejipanga vyema, imefanikiwa kumsajili straika wa Mtibwa Sugar, Nassor Kiziwa, kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hiyo ni siku moja baada ya kumtambulisha mchezaji mwingine, Michael Masinda, kutoka Prisons pamoja na Kocha Mkuu, Mohamed Abdallah 'Bares.'

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imesema wanaamini usajiliwa wa Kisiwa utakisaidia kikosi chao kufanya vizuri katika msimu ujao utakaoanza Agosti 15, mwaka huu.

Usajili huo ni moja kati ya maagizo ya Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, aliyewataka wabunge, wafanyabiashara na wasanii kutoka Kigoma kuichangia klabu hiyo kwa hali na mali ili kusajili wachezaji wazuri.

"Tuitie moyo timu yetu ili ikashindane, siyo kila siku kuziangalia Simba na Yanga kwenye TV, tunataka waje hapa, waje Lake Tanganyika...lakini kukarabati uwanja wetu ufanane na Kigoma tunayotaka kuijenga,"

## Ligi ya Mabingwa Wanawake Jumapili

**Na Saada Akida**

LIGI ya Mabingwa wa Mikoa ya Wanawake Tanzania (RWCL 2023), inatarajiwa kufanyika kuanzia keshokutwa jijini Mwanza, imeelezwa.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, amesema timu zote zilizothibitisha kushiriki ligi hiyo zinatarajiwa kuwasili Mwanza leo.

Ndimbo alisema wanaamini klabu zote zenye sifa ya kushiriki ligi hiyo zimejiandaa vyema kuonyesha ushindani kwa ajili ya kupata timu imara zitakazopanda daraja.

"Tunaamini kila timu imejiandaa vizuri, timu zote zinatakiwa kuwasili Mwanza kesho (leo), Julai 14, 2023. Baada ya kuwasili ndio maandalizi mengine yataendelea ikiwamo upangaji wa ratiba, tunaamini kila kitu kitakwenda vyema," alisema.

Timu mbili zitakazofanya vyema zitapanda daraja kucheza Ligi Daraja la Kwanza la Wanawake msimu ujao.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### HANDERSON KUMFUATA GERRARD

NAHODHA wa Liverpool, Jordan Henderson, anafikiria kuondoka katika klabu hiyo na kwenda kujiunga na Al-Ettifaq inayofundishwa na Steven Gerrard ya Saudi Arabia. Hata hivyo Waarabu hao bado hawajawasilisha ofa rasmi kwa kiungo huyo wa kati wa England, lakini wanataka kumsajili. **(Telegraph)**

### PSG YAMFUATA KANE

PARIS St-Germain itafanya kila linalowezekana kumpata mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, kwenye klabu hiyo - ingawa chaguo lake la kwanza linabaki kuwa Bayern Munich. **(RMC Sport)**

### BARCA YAMWINDA SILVA

BARCELONA inataka kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ureno, Bernardo Silva (28), lakini mpango wao mbadala ni kumnasa mchezaji wa Tottenham Hotspur na Argentina, Giovani lo Celso, mwenye umri wa miaka 27. **(Mundo Deportivo)**

### SANGARE ANUKIA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest imeendeleza nia yao ya muda mrefu ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa PSV Eindhoven na Ivory Coast, Ibrahim Sangare, mwenye umri wa miaka 25 kwa kuweka ofa mezani. **(Athletic)**

### LIVERPOOL YAMTAKA COLWILL

LIVERPOOL iko tayari kutoa ofa kwa beki wa kati wa Chelsea, Levi Colwill, mwenye umri wa miaka 20 ambaye ni raia wa England. **(90min)**

### FELIX AGOMBEWA ENGLAND

MANCHESTER United, Newcastle United na Aston Villa zote zinawania huduma ya mshambuliaji wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23. **(ABC, via Metro)**

### RICE AICHANGANYA WEST

WEST Ham iko njia panda katika mchakato wa kumuuza kiungo wa kati wa England, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 24 kwa dau la pauni milioni 105, jambo ambalo linasababishwa na kucheleweshwa kutayarishwa kwa nyaraka na mawakili wa Arsenal. **(Sky Sports)**

### DEMBELE, VARDY SOKONI

EVERTON inavutiwa na mshambuliaji Mfaransa, Moussa Dembele, mwenye umri wa miaka 27 na mshambuliaji wa Leicester, Jamie Vardy (36). **(Football-Transfers)**

### BARNES ATAJWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United bado ipo katika mazungumzo na Leicester City kuhusu winga wao Harvey Barnes mwenye umri wa miaka 25, huku The Magpies wakifikiria kutoa ofa ya awali ya takribani pauni milioni 30. **(Mail)**

### RAMSEY ANUKIA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Nice na Timu ya Taifa ya Wales, Aaron Ramsey, mwenye umri wa miaka 32 ana ofa ya fedha nyingi mezani ili kuhamia Saudi Arabia. **(Sun)**

### HOJBJERG KUTUA ATLETICO

KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, mwenye umri wa miaka 27 yuko katika orodha ya nyota wanaosakwa na Atletico Madrid. **(Marca)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BAYERN YAMWANDALIA KANE DAU LA REKODI

Hata hivyo kocha wa Spurs asema bado anaamini mshambuliaji huyo ni...

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich inatayarisha ofa ya tatu ya kumnunua mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, yenye thamani ya euro milioni 80, kwa mujibu wa 90min.

Bavaria hao wanaendelea na harakati zao za kumsaka nahodha huyo wa England, ambaye wamekuwa wakimtaka kwa muda wa miezi 12 iliyopita licha ya Spurs kusisitiza hatauzwa.

Mkataba wa Kane unamalizika mwaka 2024 na hadi sasa amegoma kusaini mkataba mpya na Tottenham kufuatia kumaliza vibaya zaidi kwenye Ligi Kuu ya England katika kipindi cha miaka 14.

Jumapili iliyopita 90min iliripoti Bayern Munich walifuata ofa zao za awali kwa Kane na ya tatu ya euro 80m - kiasi sawa na kile walichotumia kumnunua Lucas Hernandez, aliyevunja rekodi ya klabu mwaka wa 2019. Hata hivyo, Tottenham walisimama kidete na kuipiga tena.

Vyanzo vimethibitisha 90m haijawakatisha tamaa Bayern Munich na sasa wako tayari kuvunja rekodi yao ya uhamisho ili kumleta Kane Allianz Arena, na ombi la tatu litawasilishwa katika siku zijazo.

Hata hivyo, Tottenham wamesisitiza hawako tayari kufanya mazungumzo ya kumuuza Kane na wana uwezekano wa kukataa ofa yoyote kutoka kwa vigogo hao wa Ujerumani.

Kocha Mkuu mpya wa Spurs, Ange Postecoglou, alikutana na Kane kwa mara ya kwanza Jumatano wakati aliporejea Hotspur Way kwa mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya.

Tottenham wana matumaini Kane atakubali katika mipango ya Postecoglou ya kujenga upya timu na kumshawishi wa kuongeza muda wake katika klabu hiyo.

Akizungumza katika mkutano wake na waandishi wa habari Jumatatu, Postecoglou alikiri kwa sasa hajali kuhusu mazungumzo ya Kane kuondoka katika klabu hiyo.

“Ikiwa nasema inaniudhi, utakuwa upotoshaji. Kichwani mwangu hivi sasa, Harry yuko likizo, yuko kwenye kitanda cha jua na anacheza na familia yake na wakati mzuri. Hiyo ndiyo picha niliyopata.

“Sasa, ikiwa mambo mengine yanaendelea sitafikiria juu yake na sababu ya kutofikiria atakuwa hapa baada ya siku mbili zijazo (Jumatano) na kila kitu ninachohitaji kujua kitakuwa sawa mbele yangu.

“Hakuna kitu ambacho kimetua kwenye meza yangu kwa sasa kutoka kwa mtu yeyote kwenye klabu kusema kuna uamuzi utakaofanywa hapo. Hata sijakaribia hilo, kwa hiyo kwa sababu hiyo ninatazamia kuwa na Harry hapa Jumatano.”

# MAHREZ NJIA NYEUPE KUTIMKIA SAUDIA



**MANCHESTER, England**

WINGA wa Manchester City, Riyad Mahrez amebakia mchezaji anayewindwa na klabu ya Al Ahli inayoshiriki Ligi Kuu Saudi Arabia, vyanzo vimeiambia 90min.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alipoteza nafasi yake katika kikosi cha kwanza kuelekea mwisho wa msimu wa 2022/23 na hakufurahishwa na kukaa benchi wakati City wakishinda taji la FA na fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

90min ilifichua Mahrez alikuwa akiwasiliana na Al Ahli mwishoni mwa Juni, klabu hiyo ikiwa tayari kumlipa pauni milioni 45 kwa mwaka. Yeye yuko wazi kwa hatua kama hiyo.

Kama ilivyokuwa mwezi uliopita, City bado wanasitasita kumwacha Mahrez aondoke, huku mustakabali wa Bernardo Silva ukizidi kutokuwa na uhakika na ndio sababu kuu ya kutofanya uamuzi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ameomba akubaliwe uhamisho wa majira ya joto na PSG wanataka kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji wa kwanza kusajiliwa na kocha, Luis Enrique.

Mchezaji mwingine ambaye yuko kwenye rada za Saudi Arabia ni beki wa kati wa City, Aymeric Laporte.

Hapo awali iliripoti Laporte alikuwa akiwindwa na Aston Villa na Tottenham Hotspur, lakini City haijapokea ofa yoyote kubwa kutoka kwa klabu hizo.

Huku nia kutoka Ulaya haijajitokeza, City iko tayari kumuuza kwa wanunuzi walio tayari kutoka Saudi Arabia, huku Al Ahli wakiwa tayari kumpa njia ya kuondoka.

Al Ahli pia wanamtaka kiungo wa Napoli, Piotr Zielinski, ambaye anasakwa na Lazio kuchukua nafasi ya Sergej Milinkovic-Savic aliyejiunga na Al Hilal.

# Laporta: Barca ina timu bora

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, amesema timu yake ni bora kuliko wapinzani wao Real Madrid na inaweza kutwaa tena ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu ujao pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya.



Barca walirejea kwenye mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya mapema wiki hii na wamesajili wachezaji wawili katika dirisha la uhamisho hadi sasa ambao ni Ilkay Gundogan na Iñigo Martinez.

"Tuna timu bora kuliko Madrid na, mchezaji mmoja mmoja, sisi pia ni bora, na tofauti kidogo kuliko wapinzani wetu," alisema Laporta akiiambia Sport.

"Kama mwanachama na shabiki wa klabu, nimeridhishwa sana na timu tunayoijenga."

Madrid, ambao walimaliza wakiwa washindi wa pili nyuma ya Barca msimu uliopita wa LaLiga, wamewaongeza Jude Bellingham, Joselu, Fran Garcia na Arda Guler.

"Tayari tuna timu yenye ushindani," alisema Laporta.

"Tumeshinda Ligi ya Hispania na tunaweza kuendelea kutumia ubabe katika mashindano haya. Pia tunataka kuwa katika kundi la wagombea kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ninazingatia kuunda timu nzuri juu ya kusajili wachezaji wazuri. Tumewasajili Gundogan na Martinez na watatupa kiwango kizuri kama wengine wanaokuja.

"Tunamkosa beki wa kulia na tunalifanyia kazi. Pia tunataka kuimarisha safu yetu ya kiungo."

Hata hivyo, Barca walishindwa katika jaribio lao la kumrejesha Lionel Messi katika klabu hiyo.

## PSG yajitosa kumwania Felix

**PARIS, Ufaransa**

PARIS Saint-Germain inajipanga kumsajili, Joao Felix ili atue katika mji mkuu wa Ufaransa, vyanzo vimethibitisha kwa 90min.

Felix alianza mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya akirejea Atletico Madrid wiki hii, na katika mkutano na viongozi wa klabu hiyo alithibitisha anataka kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto.

90min inaelewa Felix anatamani kuhamia Paris Saint-Germain ili kufanya kazi na kocha mpya, Luis Enrique.

Enrique amewasili Parc des Princes, akichukua nafasi ya Christophe Galtier, na vyanzo vimethibitisha amemtaja Felix kama mchezaji anayetarajiwa kusajiliwa na mabingwa hao wa Ligue 1 majira haya ya joto.

Kwa hali ilivyo, Atletico Madrid wanadai takriban euro milioni 90 kwa huduma ya fowadi huyo, wakiwa wamelipa zaidi ya euro milioni 120 kumsajili kutoka Benfica mwaka wa 2019.

Kwa mujibu wa 90min PSG ingependelea mkataba wa mkopo, ikiwa na chaguo la kumnunua, lakini Atletico wanataka kumuuza jumla.

Felix alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo akiwa Chelsea, mkopo ambao haukujumuisha jukumu la kununua na klabu ikaamua kutotumia nafasi hiyo kumsajili fowadi huyo wa Ureno moja kwa moja kwa kuwa haendani na mipango ya Mauricio Pochettino pale Stamford Bridge.

Klabu nyingine za England zinazohusishwa na kumwania mchezaji huyo ni pamoja na Manchester United, Tottenham Hotspur, Newcastle United na Aston Villa.



## HABARI MICHEZO

# SIMBA SC YAMLETA NCHINI MIQUISSONE KIMYA KIMYA

**Na Saada Akida**

KIUNGO mshambuliaji wa Al Ahly ya Misri, Luis Miquissone, raia wa Msumbuji ametua nchini kimya kimya na kupokewa na mabosi wa Simba kwa ajili ya kuendelea na mazungumzo ya kumsajili kwa ajili ya msimu mpya, imefahamika.

Simba imekuwa ikihaha kumrudisha nyota huyo ambaye ilimuuza kwa mabingwa wa Afrika, Al Ahly mwaka juzi lakini hakufanikiwa kupata namba kwa Waarabu hao.

Hali hiyo ilisababisha Al Ahly kumtoa kwa mkopo katika klabu ya Abha ya Saudi Arabia, ambayo tayari amemaliza mkopo huo na kurejea kwenye timu yake 'mama'.

Taarifa zilizopatikana kutoka Simba zinasema jina la Miquissone limepitishwa katika orodha ya wachezaji wanaowindwa lakini ikimhitaji kwa usajili wa mkopo ambao wanaitaka AlAhly kusaidia kumlipa mshahara nyota huyo.

"Miquissone yupo tayari nchini na amefikia katika kambi ya Simba, na hayupo peke yake, wapo wachezaji wengine ambao hawajaenda Uturuki kutokana na uongozi kushughulikia changamoto zao ili kukamilisha taratibu za safari. Wakati wowote wanaweza kumtangaza kama mchezaji mpya wa Simba.

Unajua hakuna kitu ambacho kinawapa wakati mgumu uongozi kama lawama wanazopata kutoka kwa mashabiki, ndio maana wamekuwa makini sana", kilisema chanzo chetu.

Nipashe ilipomtafuta Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kwa sasa bado hawajatambulisha wachezaji watatu.

"Nadhani hatujamaliza, wapo ambao tutaendelea kuwatambulisha na kuna mchezaji mmoja mkubwa sana ambaye utambulisho wake nchi itaenda kutikisika," alisema Ahmed.

Aliongeza uongozi wa klabu hiyo umeahidi kuendelea kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa ambao utawapa matokeo chanya na furaha katika msimu mpya.




Katibu Mkuu wa Chama cha Waandishi wa Michezo Tanzania (TASWA), Alfred Lucas (kulia) na Mkurugenzi wa IPRT, William Kallaghe wakisaini mkataba wa ushirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo unaolenga kutoa mafunzo ya mawasiliano kwa waandishi ili kuwajengea uwezo katika kukuza na kuendeleza michezo nchini. Wanaoshuhudia ni wawakilishi wa taasisi hizo akiwamo Mwenyekiti wa TASWA, Amir Mhando (kulia waliosimama). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga, CRDB mambo mazuri

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umeingia makubaliano na Benki ya CRDB kwa ajili ya kusimamia matukio yote kuelekea Siku ya Wananchi itakayofanyika Julai 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Siku hiyo Yanga itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Kaizer Chiefs kutoka Afrika Kusini na uzinduzi rasmi wa tamasha hilo utafanyika kesho kwenye Uwanja wa Furahisha jijini Mwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Yanga, Endre Ntine, alisema wanatarajia siku hiyo kutambulisha kikosi chao kipya cha msimu wa 2023/2024.

"Ni siku muhimu sana kwa kuingia makubaliano na CRDB ya kufanikisha sherehe zetu za Siku ya Wananchi itakayofunguliwa rasmi Jumamosi, kutakuwa na mechi kubwa kati ya kikosi chetu dhidi ya Kaizer Chief," alisema Ntine.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa CRDB, Stephen Adili, alisema wanaendelea kushirikiana na Wananchi ili kufanikisha malengo yao katika kupiga hatua katika soka.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wanaendelea kuimarisha kikosi chao na wanajipanga kumtambulisha mchezaji mpya ambaye wamemsajili kujenga kikosi imara.

Kamwe alisema wachezaji wote wapya watakuwapo katika Siku ya Wananchi ambayo ni rasmi kufahamu nyota watakaoitumikia timu hiyo.

Alitaja viingilio vya Siku ya Wananchi ni Sh. 10,000 katika eneo la mzunguko huku kile cha juu cha tiketi za Royal ni Sh. 300, 000 ambapo shabiki atapata zawadi ya jezi na usafiri huku tiketi za VVIP zikiuzwa kwa Sh. 500,000.

# Chama aitikisa Simba

INATOKA UK. 24

inamtaka na yupo ndani ya klabu hiyo atabakia na endapo atakuwa nje ya timu hiyo pia itahakikisha inamsajili ili kufikia malengo.

"Wanasimba wasiwe na wasiwasi, hakuna mchezaji ambaye Simba wanamtaka, wakamkosa, kama yupo ndani ya kikosi ataendelea kuwamo na kama yupo nje ya timu tutamsajili, Simba ina pesa ya kusajili, msiwe na hofu," alisema Ahmed.

Naye Baleke aliliambia gazeti hili bado ana mkataba wa miaka miwili na Simba, hivyo mashabiki wasiwe na wasiwasi kuhusu uwepo wake.

Baleke alisema hakuambatana na kikosi cha timu hiyo kwa sababu ya kufuatilia taratibu za kisheria za kubadilisha hati yake ya kusafiria.

Mkongomani huyo amewataka mashabiki na wanachama wa Simba wapuuze taarifa za yeye kwenda kufanya majaribio katika moja ya timu za Ulaya si za kweli.

"Ninachojua mimi ni mchezaji wa Simba, mimi mtoto halali wa Simba kwa miaka miwili, hayo mambo ya mkopo sifahamu, sijaenda kufanya majaribio kama taarifa zinazosambaa, nilienda nyumbani kufuatilia hati mpya ya kusafiria. Kwa sasa nakamilisha taratibu ili wiki ijayo nianze safari ya kwenda Uturuki kuungana na kikosi kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano," alisema Baleke.

Aliongeza msimu uliopita alijiunga na Simba ligi ikiwa katikati lakini anaamini atakuwa na wakati mzuri katika msimu mpya kwa sababu ya kupata muda wa kufanya maandalizi ya pamoja mapema.

"Msimu uliopita nilifanya vizuri kwa kushirikiana na wachezaji wenzangu kupata matokeo kwa kila mechi, tuliondolewa katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, naamini msimu ujao tutafanya bora zaidi," Baleke alisema.

Aliongeza wanaenda kujiimarisha ili kutoishia hatua hiyo katika msimu mpya wa mashindano hayo ya kimataifa pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunaenda kujiimarisha ili msimu ujao tufikie malengo ikiwamo kutwaa mataji yote ya ndani na kuvuka tulipoishia katika michuano ya kimataifa," aliongeza Mkongomani huyo.



Simba ikiwa na Kocha Mkuu, Roberto Oloviera 'Robertinho' ilimaliza nafasi ya pili katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita lakini pia ikiishia hatua ya nusu fainali kwenye mashindano ya Kombe la FA.

# Michezo

Ijumaa Julai 14, 2023

Nipashe




## Bayern yamwandalia Kane dau la rekodi

UKURASA 21




Kiungo Jonas Mkude 'Nungu nungu' ametangazwa rasmi mchezaji mpya wa Yanga baada ya kusaini mkataba wa mwaka mmoja akiwa mchezaji huru. Simba ilitangaza kuachana na Mkude aliyeitumikia timu yao kwa muda wa miaka 13. **PICHA: MTANDAO**

# CHAMA AITIKISA SIMBA

●●●Klabu yafunguka mazungumzo ya kumbakisha kiungo huyo yako...

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

WAKATI kiungo Mzambia Clatous Chama amewashtua mashabiki na viongozi wa Simba kwa kugoma kwenda Uturuki akitaka maboresho ya mkataba wake, mshambuliaji wa timu hiyo, Jean Baleke, amesema yeye bado ni mali ya Wekundu wa Msimbazi.

Mkataba wa Chama na Simba umebakiza mwaka mmoja lakini kiungo huyo amesema menejimenti yake imepokea ofa kutoka katika timu nyingine zilizoko nje ya Tanzania.

Hata hivyo imeelezwa uongozi wa Simba umemtaka Chama kuwasilisha ofa hizo au kuzitaja timu zinazomhitaji jambo ambalo nyota huyo amekataa kuweka hadharani.

Taarifa kutoka Simba zinasema klabu hiyo imeshaanza mazungumzo na Chama na endapo mambo yataenda sawa atasaini mkataba mpya na baadaye kuelekea katika kambi iliyoko Uturuki ili kuungana na wachezaji wenzake.

"Bado mazungumzo yanaendelea, ni kweli Chama alikuwa na mahitaji ya kuboreshwa maslahi yake, mazungumzo yanaendelea vyema na kama mambo yataenda vizuri muda wowote ataondoka kuelekea Uturuki," alisema kiongozi mmoja wa Simba.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema mashabiki wa Simba hawapaswi kuwa na wasiwasi kwa sababu mambo yapo shwari na wasikubali kuondolewa kwenye 'reli' na wapinzani wao.

Alisema kila mchezaji ambaye Simba

UKURASA. 23

# Kipenga Ligi Kuu kuanza Agosti 15

**Na Faustine Feliciane**

SAFARI ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu mpya wa mwaka 2023/2024 inatarajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu kwa kushirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, imefahamika.

Yanga ya jijini Dar es Salaam ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo ya juu nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), ligi hiyo itaanza siku mbili baada ya kumalizika kwa mechi ya kusaka bingwa wa Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 13, mwaka huu.

Bodi ya Ligi ilisema msimu wa 2023/2024 unatarajiwa kumalizika ifikapo Mei 25, mwakani na imepangwa kwa kuzingatia ushiriki wa timu nne kutoka Tanzania Bara zitakazopeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Michuano hiyo ya Ngao ya Jamii itahusisha timu nne zitakazocheza mtoano kupata timu mbili zitakazocheza fainali ya kusaka bingwa mpya ambayo ni ishara ya kuanza kwa msimu mpya.

Michezo hiyo imepangwa kufanyika kuanzia Agosti 9 hadi 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani jijini Tanga.

Timu zitakazoshiriki kuwania Ngao ya Jamii ni bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika, Yanga, mshindi wa pili ambaye ni Simba, Azam FC iliyomaliza nafasi ya tatu na mshindi wa nne, Singida Fountain Gate.

Katika kuwania taji hilo, Yanga itacheza dhidi ya Azam FC wakati Simba itaumana na Singida Fountain Gate kwenye mechi za hatua ya nusu fainali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >